
Washa
Injini Zenu
Kitabu cha Mwalimu

# Washa Injini zenu

*Je! uko tayari kwa mbio ya kiroho?*
*1 Wakorintho 9:24*




**Programu ya Shule ya Likizo ya Biblia kutoka kwa "Watoto ni muhimu"**

**Kitabu cha Mwalimu kwa miaka yote**

Wavuti: www.ChildrenAreImportant.com/engines/

## Shukrani Kwa Wote katika Timu ya "Watoto Ni Muhimu!"

Mhariri: Kristina Krauss

Timu ya Ubunifu: Abril Palacios Camacho, Areli Zuriel Salinas Sanchez, Dwight Krauss, Jennifer Sánchez Nieto, Julio Sánchez Nieto, Mike Kangas, Monserrat Duran Díaz, Suki Kangas, Verónica Toj, na Vickie Kangas.

Shukrani kwa Rubén Dario kwa muziki wa ajabu katika programu hii.

Timu ya Tafsiri: alineviera, Annupama Wankhede, Anton Klymyk, Araz Mammadzadeh, Aroma Publications and Media, Arturo Jr Boron, Blessy Jacob, Carmela Dawn Flores, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, HamidReza Azimi (hamid.azimi1364 at gm#ail com), Heyaudrey, I-clever.com, iqbalman, Jacob Kuruvilla, kamilturk, Karunguru Mwangi, kiran, Maitrayi Mondal, Marco Chu, Marcos Rocha, Mathew Das, Mitesh Mandaliya, mrramlama, Mrs.Geethashree NavaneethaKrishnan, Nassim Bougtaia, nicbenk, Paul Mwangi, Paul Septan, Rana922, Rubina Rai, Safdar Khan, shahroshan15, Talento-Unido, ueritom, Verdia Juliansyah Cancerika, Yeoh Jung Chin, Zeina Mirella Barzaga Arencibia

# Karibu kwenye VBS
# Washa Injini zenu!

Kulingana na Biblia, safari yetu pamoja na Kristo sio tu tukio linaloendelea bila kujali; ni mbio! Sisi pamoja na watoto tunapaswa kujitahidi ili tushinde, na kushinda mbio hii hakutatukabidhi tuzo la duniani ambalo litazeeka au kupotea kwenye kabati, lakini malipo ya milele:

"Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika." 1 Wakorintho 9:24-25

Kuna malipo ya milele kwetu ikiwa tutasisitiza kwa bidii na kumfuata Yesu Kristo kwa kila kitu tulicho nacho! Katika VBS hii inayohitaji nguvu na kasi, tutashuhudia mashindano ya pikipiki kama mfano wa maisha yetu katika Yesu Kristo.
Kama ilivyo kwa gari lolote lenye injini, pikipiki lazima iwe katika hali bora zaidi ili kushindana katika mbio. Injini inahitaji mafuta kufanya kazi, vinginevyo itaharibika! Kwa njia hiyo hiyo, kama wafuasi wa Yesu, tunapaswa kujizoesha kukubali makosa yetu na kujuta kila wakati tunapofanya jambo baya. Pikipiki inahitaji matairi mapya kwa mgusano mzuri ili kukimbia kwa haraka kwenye barabara. Kwa njia hiyo hiyo, ni lazima tujizoeshe utiifu ili tupate mgusano mzuri kwa kufuata Yesu katika maisha yetu. Kama bidhaa ya kudhibiti halijoto inavyohitajika katika injini ili kuiweka bila joto au baridi nyingi, tunahitaji kujizoesha upendo wa Kristo kwa wengine katika maisha yetu, ili kutusaidia tuepuke kuchanganyikiwa na ugomvi na ndugu zetu katika Kristo. Kama gari lisilo na mafuta, hatuwezi kufanya chochote bila nguvu ya Kristo katika maisha yetu. Na hatimaye, katika shindano kubwa la pikipiki kutakuwa na kituo cha kusimama kilicho na timu ya watu ambao watafanya kazi pamoja ili kutunza pikipiki na kuiweka katika hali bora zaidi wakati wa mbio. Atakayesimamia timu hii ni msimamizi ambaye kazi yake sio tu kuangalia ufundi wa gari, lakini pia kufuatilia shindano na kuelekeza dereva katika vikwazo vyovyote. Kama mkuu wa mbio, Yesu Kristo anashughulikia mambo haya yote na hutuelekeza kama kiongozi wetu wa timu. Wewe na timu yako ya VBS mnaweza kuzindua tukio hili kwa kutumia mawazo kutoka kituo cha "Ubunifu wa Gereji," michezo kwenye kituo cha "Tayari, Anza, Michezo!", mawazo ya kutengeneza vitafunio kutoka kwenye Sehemu ya Kitafunio, na vitabu kwa wanafunzi vilivyo na shughuli za kujifurahisha na mafumbo katika Darasa la Uendeshaji. Kukutana na mhusika wa Fundi wa Gari katika mchezo.Fundisha masomo yenye ucheshi ambayo yanajumuisha ulinganifu wa mbio na hadithi ya Biblia na kujifunza baadhi ya maneno katika lugha ya ishara ili kuifanya iwe ya kuvutia kwa watoto. Tumia mbinu ya kuwa umakini kila siku ili kuongeza hamu, na usisahau nyimbo zenye vitendo! VBS hii ni chombo kikubwa cha uinjilisti, basi aalika watoto wengi iwezekanavyo kwenye VBS yako. Hadithi ya kibiblia katika Somo la 5 ni kuhusu jinsi Yesu alivyofariki msalabani na wokovu. Usisahau kuwaalika watoto kukubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao!

"Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu." *Waebrania 12:1*







Mungu akubariki sana unapowafundisha watoto wako kumfuata Kristo kwa unyenyekevu, utiifu na upendo, na kumweka Yesu Kristo kama kiongozi wa timu yako. Tunatumai kwamba watoto wengi watamkubali Kristo, na kwamba itakuwa baraka kubwa kwa kanisa lote. Haya twende!

Baraka nyingi kutoka kwa timu ya ubunifu ya Watoto ni Muhimu!









# Jinsi ya kutumia VBS hii

## Kwa Mwelekezi Pekee

Kama mwelekezi wa programu, tunakushauri usiwe kiongozi au mwalimu wa timu au darasa lolote, lakini uweke watu wengine katika kila sehemu ya kazi. Wakati kuna tatizo kuhusiana na rasilimali zilizopotea, ajali kwa mtoto, mwalimu anayekosekana au haja ya kuzungumza na mchungaji mkuu, hii itakuwa jukumu lako wewe kama mwelekezi.Huwezi kufanya kazi yako inavyopaswa ikiwa utajishughulisha na mambo mengine kama uhubiri wa ujumbe mkuu au kuandaa vitafunio. Waachie wenzako kanisani kazi hii ya kusisimua.

## Wajitoleaji

Kupata watu ili kukusaidia katika VBS ni rahisi zaidi kuliko Shule ya Jumapili kwa sababu VBS inafanyika kwa wiki moja tu.Jaribu kuhusisha wajitoleaji wengi , kwa sababu kufanya hivyo kutahamasisha washirika.
Kagua kazi zinazopatikana ili kutekelezwa na wafanyakazi.Baada ya kufanya hivyo, tafuta watu wenye ujuzi sahihi ili kukusaidia.Chagua watu wanaopenda watoto, ambao wanaaminika na wanaingiana na wahusika.
Hatua inayofuata ni kwenda kwao moja kwa moja na uwaalike wafanye kazi maalum katika VBS. Shiriki maono ya kufikia watoto wa eneo la karibu kwa ajili ya Kristo mkiwa pamoja nao.Mara nyingi watu hujitolea kikamilifu wanapoalikwa binafsi.

## Maombi

Anza kupanga Shule ya Likizo ya Biblia ya (VBS ) kwa maombi.Tenga muda wa kuzungumza na Mungu , kutafuta uelekezaji Wake unapopanga tukio lako.Mwombe rafiki yako wa karibu aombe mnapokaribia wiki ya tukio. Kusanya timu yako na mwombe pamoja na mchungaji wako.

- Tafuta watu watakaosimama nanyi kwa maombi wakati wa VBS.
- VBS ni fursa nzuri ya kujifunza kwa watoto wa kanisa lako na pia chombo cha uinjilisti.Usipuuze umuhimu wa maombi kwa ajili ya tukio hili.

*"Maombi ya mtu mwenye haki yana nguvu na huleta matokeo."* (Yakobo 5:16)

## Mafunzo

Tengeneza ratiba ya kikao cha mafunzo ili kufundisha wote watakaohusika katika VBS. Katika siku hiyo utaweza kuwaelezea kwa undani jinsi mpango utakavyofanya kazi na utawapa majukumu kwa kila mmoja.

## Kuchagua Tarehe na Mahali

Chagua tarehe inayofaa kulingana na kalenda ya kanisa. Mara baada ya kukubaliana na mchungaji wako, thibitisha kwamba hakutakuwa na shughuli zingine katika jamii yako wakati huo
ambazo huenda zikaingiliana na VBS. Si lazima uwe na VBS kanisani.Pia una fursa ya kufanya VBS yako katika bustani katika eneo jirani au mahali pa umma ili kufikia watoto zaidi.Unapochagua mahali, kumbuka kwamba unapaswa kuratibu muda wa kuweka mapambo na kusafisha nafasi.
Mpango huu umetengenezwa kama VBS ya siku 5, lakini unaweza kuurekebisha kulingana na mahitaji yako .Inaweza kuwa VBS ya siku 3 pekee kwa kutumia masomo ya 1, 4 na 5, ikiwa utachagua hilo .Nyenzo imetengenezwa ili ikufae, sio kanuni kali ambayo lazima ufuate.







## Matangazo

Unaweza kuanza kutangaza kwa takriban wiki 4-6 kabla ya tukio hilo. Hakikisha imetangazwa kutoka mimbari ya kanisani na uhakikishe kwamba umewasiliana kuhusu maono ya kufikia watoto katika jamii.

• Shule ya likizo ni hatua nzuri ya kwanza ya uinjilisti, kwa sababu huenda watu wanaweza kuogopa kuhudhuria kanisa pamoja na watoto , lakini hakuna mtu atakayepinga kutuma watoto wake katika mpango wa wiki kwa ajili ya watoto wakati wa likizo.Hii inatoa fursa kwa familia zitakazomtembelea, na hata wazazi wanaweza kuhudhuria ili kuona kile ambacho watoto wao wanafanya.Hii inawatia changamoto washiriki ili kuwaza kuhusu familia ambazo wanaweza kualika.

• Waalike watu ili washiriki katika kutangaza kwa kusambaza mialiko, vipeperushi, nk. Hakikisha una vifaa vya matangazo vya kutosha.

• Weka baadhi ya mabango katika maeneo tofauti (maduka, maeneo ya umma). Unaweza hata kuwa na shindano la kumzawadi mtu ambaye ataleta wageni wengi zaidi kwenye VBS. (Tuzo inaweza kuwa chakula cha jioni au kitu kingine).




## Usajili

Himiza usajili kabla ya tukio lako. Hii itakusaidia ubaini idadi ya watakaohudhuria ili uweze kupanga kuwa na nyenzo za kutosha kwa kila mtu. Kumbukumbu nzuri pia itasaidia kuweka orodha ya watoto na familia kwa ajili ya matukio mengine ya uijilisti ya baadaye.

## Vituo vya Mzunguko

Unaweza kutumia VBS hii kulingana na mapendeleo yako, lakini imeundwa ili itumike katika mpango wa mzunguko wa vituo vitatu kwa wakati mmoja.Hii inamaanisha kwamba unafaa kugawanya watoto katika vikundi vitatu, na vikundi vinazunguka kupitia vituo vitatu, hata kama vituo vyote vinapatikana katika sehemu moja.Kila kituo kitadumu kwa muda wa dakika 20 hadi 40, na kila kituo kinarudiwa mara tatu ili kila kikundi kiweze kwenda katika kila kituo mara moja kwa siku. Njia rahisi ya kugawa watoto ni kulingana na umri, na hii pia husaidia wakati wa kutumia vitabu vya mwanafunzi:

• Rahisi (miaka 4-6)
• Wastani (miaka 7-9)
• Ngumu (miaka 10-12)

Tuna kikundi kingine cha Umri wa juu (miaka 13+) ikiwa watoto wako wakubwa wangependa kushiriki katika VBS. Unaweza kugawa makundi kwa ajili ya vituo vya mzunguko kulingana na idadi ya wanafunzi katika kila kikundi cha umri, au uwe na vituo vya Darasa na Ubunifu pekee wakati shughuli ya Michezo ikifanyika mwishoni mwa siku.

Njia tunayopendekeza ya kuzunguka vituo ni kucheza muziki wakati wa kubadili, ili kuwe na msisimko wakati wanafunzi wanahamia kutoka kwenye kituo kimoja hadi kingine. Manufaa ya kutumia vituo ni kwamba walimu hawataandaa mambo mengi sana, lakini wataandaa sehemu moja ya darasa, na kurudia mara tatu.(Inakuwa kazi kidogo kwa kila mwalimu).

## Ratiba ya Mzunguko

Wote pamoja katika kikundi kimoja:

- Ufunguzi
- Muziki
- Mchezo wa Kuigiza
- Ujumbe mkuu
- Mchezo wa kujuana
- Somo la Kibiblia

Vituo vya mzunguko:

- Shughuli za Kitabu cha Mwanafunzi
- Ubunifu wa siku
- Michezo (au ucheze mchezo na kila mtu mwishoni)

Wote pamoja katika kikundi kimoja:

- Kitafunio
- Muziki
- Kufunga




## Ratiba ya Kienyeji

Wote pamoja katika kikundi kimoja:

- Ufunguzi
- Muziki
- Mchezo wa Kuigiza
- Ujumbe mkuu
- Mchezo wa kujuana

Muda katika darasani:

- Somo la Biblia
- Vitabu vya Wanafunzi
- Ufundi:
- Kitafunio

Pamoja katika michezo

Wote pamoja katika kikundi kimoja:

- Muziki
- Kufunga

## Michezo ya Kujuana

Michezo ya kujuana ni michezo mifupi ambayo unaweza kucheza na wanafunzi wako wakati wao wa ziada. Hatua hii itasaidia wanafunzi kuunganisha na kujuana na kila mmoja katika mazingira ya kikundi. Michezo ya kujuana

pia inaweza kusaidia kuboresha mafundisho kwa kuhimiza ushirikiano na uchangiaji. Inaweza kutoa himizo nzuri kwa ajili ya uchunguzi na majadiliano katika vikundi vidogo kwa:

- Kusaidia watu katika kundi jipya kujuana.
- Kusaidia washiriki wapya wajiunge na kikundi.
- Kuwasaidia vijana wahisi bila wasiwasi wakiwa pamoja.
- Kuhimiza ushirikiano.
- Kuhimiza kusikiliza wengine.
- Kuhimiza kufanya kazi kama timu.
- Kuhimiza vijana kuacha makundi waliozoea
- Kuendeleza ujuzi wa kijamii.
- Kujenga uhusiano na viongozi.
- Kujenga mazingira mazuri ya kujifunza na kuchangia.

Wanafunzi wako hawatapendelea kusikiliza hadithi ya Biblia moja kwa moja baada ya kusikilizaa ujumbe mkuu!Itachosha wakati mazungumzo na mahubiri yanafuatana . Tumegawanya "mazungumzo" na mchezo ya kujuana katika kila somo. Tumia michezo hii uwasaidie wanafunzi wako wasalie makini na wajifunze somo kila siku!

## MICHEZO

Kuna michezo mawili iliyotolewa kwa kila somo kwa watoto wa shule katika nyenzo hii. Mchezo mmoja ni wa muundo wa kubadilishana katika timu, na mchezo mwingine ni wa mtu binafsi, ambapo watoto wanashindana na mshindi atakuwa mtoto mmoja.Unaweza kutumia michezo ili kuongeza msisimko katika VBS ili watoto wapate hamu ya kurudi kila siku.Ikiwa unapendelea, unaweza kupanga vikundi na kutoa pointi kwa timu zinazoshinda michezo.

# Mawazo ya Ziada

## Mapambo ya Mlango

Pamba mlango wa darasa lako ili mstari wa kumaliza uwe sehemu ya mwanzo wa darasa lako, au upambe kwa pikipiki zinazowakilisha kila mmoja ya watoto katika darasa lako. Unaweza kutumia ujenzi na karatasi nyingine maalum ili kupamba.






## Taa ya Barabarani

Unaweza kuunda mwenyewe.
Unahitaji tu:

- Sanduku la kadibodi
- Baadhi ya mikebe
- Kijiti cha kushikilia





## Pazia za karatasi

Ziweke kwenye milango au madirisha.

## Puto

Pamba darasa kwa miundo tofauti ya puto kama vile pia, taa za trafiki, matairi au tao ili kuwa na mazingira inayofanana na mbio halisi.









## MIDUARA YA KARATASI

Unda hizi kutoka kwa rangi au miundo inakufaa zaidi, kwa kutumia ukubwa tofauti.







## ISHARA ZA BARABARA

Zitaongeza msisimko na kusaidia kuleta mazingira mwafaka.




## SELFI YA MOTO

Hii ni fursa nzuri ya kupiga picha za watoto.




## PIKIPIKI

Unaweza kuunda hii kwa kutumia masanduu ya kadibodi pekee.




## TIRES

You can decorate with recycled tires just by adding details.





# 1 KUTAMBUA DHAMBI YANGU

Hadithi ya Biblia: Petro Anatubu / Mathayo 26:69-75, Yohana 21



## FUNGU

“Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1 YOH. 1:9

## MCHEZO WA KUIGIZA

**Fundi wa Gari Mdanganyifu**

> **KUPATA UMAKINI**
> Msemaji: “Ni wakati wa mbio!”
> Watoto: “Beep! Beep! Beep-beep!” (ngumi inagonga kwa nguvu katika kila beep) “Oooooooh” (mikono inanyoroshwa chini na kusonga juu kwa mara tatu) “Ndio!” (mikono inasonga mara moja nyuma katika sehemu ya kishikio cha pikipiki)

• Fundi wa gari anaingia, anasafisha mafuta kutoka kwa mikono yake kwa kitambaa na kucheka kwa sauti kubwa. Anaketi kwenye sofa na kuanza kunywa kinywaji. Anawaambia watoto jinsi maisha yake yalivyo: Yeye ni fundi hodari wa gari anayeitwa Bwana Oili.Anawaambia pia kuwa ana mke mrembo , binti mzuri lakini anayeasi , mbwa mzuri sana na mtiifu, na anaelezea ambako anaishi.(Taja mji katika eneo lako)
• Anaanza kucheka tena, amefurahi sana, kwa hivyo anataka kushiriki na watoto kile ambacho kinamfurahisha. Kitu fulani kilichotokea siku 10 zilizopita; mteja alileta gari lake ili libadilishwe oili.Badala ya kumpa mafuta mapya, yenye ubora na ya gharama kubwa zaidi, alimpa oili iliyotumika. Alidhani kwamba mtu huyo hangeweza kugundua na hivyo angepata fedha zaidi.
• Wakati huo, mteja anaingia, amejawa na hasira na anakimbia akielekea kwa fundi wa gari, tayari kumpiga. Fundi wa gari anaruka na kujificha nyuma ya sofa. Wao wawili wanakimbizana kwa muda mbele ya watoto katika vita, wakipiga kelele, fundi wa gari anasema kwamba yeye hakufanya chochote kibaya.
•Mteja anayepiga kelele anamwambia fundi wa gari kwamba kwamba injini yake iliharibika asubuhi, na kila mtu alipoikagua, kila mtu alisema kwamba iliharibika kwa sababu oili haikuwa imebadilishwa kwa muda mrefu. Mteja alisisitiza kwamba alikuwa amebadilisha oili, lakini hakuna mtu aliyemwamini kwa sababu oili ilikuwa imetumika sana. Mteja huyo anaendelea kumkemea fundi wa gari na kusisitiza kwamba lazima abadilishe injini hiyo kwa nyingine mpya. Wote wawili wanatoka nje wakipiga kelele na kukimbia. Mmoja wa walimu anakuja na kusema, "baadaye tutaona mwisho wake."
•Mtu anapita akiwa na ishara ambayo inasema, "Baadaye..." Sasa fundi wa gari anaingia kama anaomba msamaha, akizungumza na mteja. Bwana Oili anakubali kwamba alitumia oili iliyokuwa imetumika na anaomba msamaha kwa mteja.Anajitolea kubadilisha injini na nyingine mpya, ili kufidia makosa aliyofanya.
• Mteja anakubali na kumsamehe fundi wa gari. Wanakaribiana na kukubatiana.Fundi wa gari anampiga rafiki wake mpya kikofi mgongoni naye mteja anafanya vivyo hivyo tena kwa nguvu kidogo.Kwa wasiwasi kidogo, lakini







akiendelea kucheka, fundi wa gari anampiga kikofi chenye uzito zaidi, na kisha mteja anajibu kwa kikofi chenye uzito zaidi. Wawili hao wanaanza kucheka na kuondoka.

## UJUMBE

Watoto, karibu kwenye mwanzo wa VBS hii maalum, "Washa Injini zenu!"
Leo tutaangalia umuhimu wa oili katika injini.Katika pikipiki, au gari lolote, oili ni ya umuhimu sana, kwa sababu ikiwa utaanza kuendesha bila oili, unaweza kuharibu injini nzima! Hii itakufanya ukwame kabisa.Inasikitisha sana kupoteza injini nzima, ilhali ulichopaswa kufanya ni kukagua oili na kuhakikisha inatosha.Oili katika injini huendelea kuchafuka zaidi na zaidi kwa wakati, basi kwa wakati fulani tunapaswa kubadilisha na kuweka oili mapya.Mara kwa mara kukagua oili, wakati mwingine itakubidi ununue oili zaidi, lakini unaokoa muda na pesa ambazo ungetumia ikiwa ungeishiwa na oili na kuharibu injini.



Kuingia katika dhambi kubwa ni kama kuharibu injini ya magari yetu. Dhambi nyingi zina athari kubwa, hata baada ya Mungu kutusamehe. Dhambi zingine zitakufanya ufungwe jela kwa muda mrefu, zingine zitasababisha familia yako ikufukuze nyumbani, na zingine zitafanya uache shule. Njia bora ya kuepuka makosa haya yenye gharama kubwa ni kuwa tayari kukubali kwamba tumekosa, hata katika mambo madogo.
Hakika hakuna mtu hupenda kukubali kwamba amefanya kitu kibaya. Hali yetu ya kibinadamu hutufanya tufikiri kwamba tuko sawa wakati wote, na kwamba hatuwezi kufanya makosa. Lakini hilo sio kweli. Tunafanya makosa wakati wote, na pengine makubwa zaidi kuliko wengine. Leo tutajifunza kuhusu mtu katika Biblia, Petro, ambaye alifanya makosa.Alipatikana akifanya dhambi, na kama angeendelea kutenda hili, angeweza kuharibu maisha yake.
Badala yake, Petro alikubali dhambi yake na kutubu mbele ya Mungu. Hatua hii ilimrudisha kwenye mbio ya maishani na kumrudisha kwenye barabara. Petro akawa mtu mwenye nguvu wa Mungu. Mungu anakupenda na ana mipango maalum juu ya maisha yako. Anataka uwe mwanamume au mwanamke mwenye nguvu ndani yake, kama vile Petro katika Biblia.
Lakini ili wewe na mimi tushinde mbio hii, tunapaswa kujifunza kutoka kwa somo la Petro; kukubali wakati tunakosa na kutubu. Ili kushinda, tunapaswa kukubali kwamba tumekosa kabisa na kwamba sisi sio wakamilifu. Kisha tukiri dhambi zetu kwa Mungu. Atasamehe dhambi zetu na kututakasa, na kufanya iwe rahisi sana kusalia wasafi na kumfuata Mungu.
Lakini kwa kuwa sisi si wakamilifu, tunatenda dhambi tena na kuanza mchakato tena. Kama pikipiki ambayo daima itahitaji oili mpya katika injini yake, wewe na mimi daima tunahitaji kutambua dhambi zetu mbele za Mungu. Hili sio tukio la wakati mmoja, lakini ni mazoezi ya mara kwa mara ambayo tunapaswa kuzoea ikiwa tunataka kushinda mbio. Sisemi kwamba wokovu unafanywa mara kwa mara, lakini kuhusu KUKUBALI KWAMBA UMEKOSEA. Kitendo hiki kitaweka "oili" katika injini yako ikiwa safi, na utaenda mbali zaidi katika mbio ya maisha!

## MICHEZO YA KUJUANA


**Kikapu cha Matunda Kimepinduka**

Katika mchezo huu wa kujuana, nia ni kujua majina ya wanafunzi wanaohudhuria VBS; wazo nzuri ni kujumuisha kila mtu anayeshiriki katika VBS. Fanya watoto waketi katika safu na utapunguza tatizo wakati wa kufanya shughuli hii.
Kila mwanafunzi atakuwa katika mstari atasema jina lake kwa sauti kubwa. Watu katika safu ya kwanza na safu ya mwisho wanapaswa kuwa makini na majina.Mwalimu atalenga mshiriki fulani na kusema jina la tunda kama vile chungwa, limao, malenge, tikiti, kikapu cha matunda.Mshiriki atapaswa kusema jina la mwenzake, kulingana na kile tunda linarejelea.

**Mfano:**
Chungwa: Jina la mwenzako upande wa kulia
Limao: Jina la mwenazako upande wako wa kushoto
Malenge: Sema jina lako mwenyewe
Tikiti: Jina la mtu aliye mbele yako
Kikapu cha Matunda: Kila mtu anabadilisha mahali alipo
Unaweza kutembea kati ya safu ili kulenga wanafunzi au wafanyakazi washiriki. Sehemu ya kusisimua zaidi ni pale unasema "kikapu cha matunda kimepinduka" na kufanya kila mtu ahame.

## Somo la Biblia

Petro Anatubu




1. Petro alikuwa mwanafunzi wa Yesu, hii ina maana kwamba alikuwa mtu ambaye alimfuata Yesu ili kujifunza kutoka kwake.Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Njooni na mnifuate."Petro alimpenda Yesu sana. Alikuwa mojawapo ya wanafunzi wa kwanza ambao walimwambia, "Wewe ni Mwana wa Mungu."
Kwa neno, mwanafunzi: Funga mikono yako, uiweke mbele na wakati unaishusha chini, ifungue.



2. Baada ya kuwa pamoja na wanafunzi wake kwa miaka 3, aliwajulisha kwamba angekamatwa na baadaye angefariki.Yesu pia aliwaambia wanafunzi wake kwamba watamkimbia na kwamba watasema hawamjui.Petro akasimama na kusema: "Sitasema kamwe kwamba sikujui," na wanafunzi wengine wote wakasema pia, "Hatuwezi kamwe kusema kwamba hatukujui."
Kwa neno, kamwe: Geuza mkono wako katika nusu mduara na ushushe mkono wako upande wa kulia.

3. Mambo matatu yaliyotendeka jinsi Yesu alivyowaeleza. Askari waliwasili na kumkamata Yesu. Wanafunzi wote wakatoroka, lakini Petro alimfuata kwa mbali ili kuona nini kitamtendekea.Wakati Yesu alipokuwa akihojiwa katika nyumba ya Kuhani Mkuu, Petro alikuwa nje alijipasha joto karibu na moto kwa sababu kulikuwa na baridi kali, ghafla msichana aliyekuwa mtumishi akamwambia, "Wewe ulikuwa pamoja na Yesu," basi Petro akajibu, "Sijui unamaanisha nini."Msichana mwingine akamwambia mtu kwa sauti kubwa: "alikuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu," naye Petro akajibu, "Mimi si mmoja," (hata wakati alipokuwa amekiri kwamba hangemkana kamwe). Muda mfupi baadaye mtu akasema, "Nina hakika wewe ni mmoja











wa wanafunzi wake, umetoka Galilaya," Petro akasema maneno machache mabaya, kisha akasema, " Sijui unamaanisha nini."
Kwa maneno, sijui: Weka vidole vya mkono wako wa kulia kwenye paji la uso na uvigeuze juu.



4. Wakati huo tu, jogoo akawika; Petro akakumbuka yale Yesu aliyomwambia, "Kabla jogoo awike utakuwa umenikana mara tatu." Petro alianza kulia kwa sababu mbele ya wanafunzi wengine alikuwa amesema kwamba hawezi kamwe kusema kwamba hakumjua. Na sasa ilikuwa mara tatu alikuwa amefanya hivyo. Petro alisikitika sana. Petro alitambua kilichokuwa kimetendeka visivyo. Pengine Petro aliuliza, "Sasa nitafanya nini? Sijui nifanye nini".
Kwa neno, jogoo: Weka kidole cha gumba cha mkono wako wa kulia kwenye paji la uso wako, uinue vidole viwili vinavyofuata.

5. Masaa machache baadaye, Yesu alisulubiwa. Alikufa msalabani ili alipe bei ya dhambi. Wanafunzi wote walihuzunika sana, lakini, Petro alikuwa wapi?Alikuwa amejificha, akitubu na akiogopa. Alikuwa amefanya kitu kibaya. Siku tatu baadaye, Yesu akafufuka tena (akawa mwenye uhai tena). Hakuwa msalabani tena, wala hakuwa kwenye kaburi, na mojawapo wa mambo ya kwanza ambayo Yesu alisema ni kwamba wao wawajulishe wanafunzi na Petro kwamba wakutane naye katika Galilaya.
Kwa neno, msalaba: Kwa vidole vyako vikiwa vimekunjwa kuelekea upande wa ndani na kidole gumba kikikwa kimeelekezwa upande wa nje, unda msalaba, kwanza kutoka juu hadi chini na kutoka kushoto kwenda kulia.





6. "Sawa, hivyo ni vizuri," akasema Petro na akaanza kuhisi vyema.Wakati Petro alikuwa karibu na Yesu angehisi furaha kuu. Siku zote hizo, Petro aliwaza," Sijui cha kufanya." Siku moja wakiwa Galilaya, Petro aliwaambia wanafunzi wengine, Mimi nitakwenda kuvua samaki, nao wakaenda pamoja naye. Waliingia ziwani na wakajaribu kuvua samaki usiku wote, lakini hawakukamata kitu chochote. Mtu mmoja aliyekuwa katika ukingo wa bahari akawaambia warushe wavu upande wa kulia (bado kulikuwa na giza, hivyo hawakumfahamu mtu huyu). Waliporusha upande wa kulia, wakakamata samaki wengi.
Kwa neno, samaki: Mikono yako ikiwa imefungwa, weka mkono wa kushoto kwenye mkono wa kulia na uisongeshe kutoka juu hadi chini.

7."Ni Bwana," Yohana akasema kwa sauti. Wakati Petro alisikia hilo, akaruka ndani ya maji na kuogelea kuelekea kwa Yesu kwa kasi zaidi.Yesu alitaka Petro ajue kwamba alikuwa amemsamehe. Yesu akamwambia Petro, "Lisha kondoo wangu, uwalishe wanakondoo wangu." Yesu alitaka Petro awaambie wengine kuhusu upendo wake kwake. Bado Yesu hakuwa amemalizana na Petro, alikuwa anataka kufanya mambo makuu katika maisha yake. Bora zaidi, Petro alijua kwamba Yesu alikuwa amemsamehe na kwamba angeweza kuanza maisha upya.
Kwa neno la kusamehewa: Kunja mkono wako wa kushoto kwa vidole vya mkono wako wa kulia.







8. Unaweza kutumia hadithi hii katika maisha yako kwa sababu wewe, pia, ni mwanafunzi wa Yesu, kama vile Petero, na unafuata njia hii. Kamwe hujachelewa kukiri dhambi zako kwa Yesu.Hata kama pia unasema " Sijui cha kufanya," jambo muhimu ni kwamba hutandanganya na hutajificha.Pengine hakutawahi kuwa na jogoo mwingine karibu nawe wa kukumbusha dhambi yako, lakini sasa unajua kwamba Kristo alikufa msalabani ili akusamehe dhambi zako zote. Na sasa Anataka uwe mvuvi wa wanadamu. Sehemu bora ya kukiri ni wakati Yesu anaruka juu kwa furaha na kukusamehe.
(Vitendo vyote)

# VITUO VYA MZUNGUKO

**Gawanya katika vikundi 3 ili waende kwenye vituo**

## USANIFU WA GEREJI

Barabara ya Mbio za Magari
Sambaza kwa kila mwanafunzi:
Karatasi 1 ikiwa na njia iliyochapishwa
Vibanzi vya msumeno na/au mapambo ya kumetameta



- Kata au uondoe mistatili na madereva wa pikipiki.
- Chukua mistatili na ukunje juu ya mistari uliowekwa katika mwelekeo mmoja, na kuunda vichupo viwili kwa kila mstatili.
- Weka gundi kwenye vichupo vilivyokunjwa, na ushikanishe kwenye njia yako popote unapotaka, na uunde daraja ndogo.
- Weka gundi kwenye barabara yako yote, halafu uongeze vibanzi vya msumeno na/au mapambo ya kumetameta ili kuiga barabara ya mbio za magari.
- Hatimaye, paka rangi madereva wako wa pikipiki, cheza nao au uwashikanishe kwenye barabara yako.

## SEHEMU YA VUTAFUNIO

Kitindamlo cha Chokoleti/Kastadi na Vidakuzi



Viungo:
- Kitindamlo cha Chokoleti/Kastadi
- Vidakuzi
- Kijiko cha plastiki

Maagizo:
1. Fungua kitindamlo cha chokoleti/kastadi
2. Fungua kifurushi cha vidakuzi
3. Vunja vidakuzi kuwa vipande vidogo
4. Weka vipande vya vidakuzi kwenye kastadi
5. Koroga vidakuzi kwenye kitindamlo/kastadi kwa kijiko

*Sasa unaweza kufurahia kukula uchafu kama mtu akiwa safu ya mbele!*

## Darasa la Uendeshaji

Karibu kwenye "darasa la uendeshaji gari" ambapo tutatumia vitabu vyetu vya wanafunzi.Je, tunaweza kuanza darasa kwa kurudia kwa pamoja somo la siku na fungu la siku?Tuanze!!!

## Maswali na majibu

1. Nini hutokea ikiwa sitaki kutubu?

Katika moyo wako hakutakuwa na amani kwa sababu Mungu katika neno lake anatuita ili tutubu, naye anatusamehe na kututakasa jinsi alivyofanya katika Biblia.

2. Je, naweza kuomba msamaha wakati wowote na popote?

Bila shaka, ni mojawapo ya mambo mazuri tunayoweza kufanya. Iwe uko shuleni au umetembelea rafiki yako, Mungu anakusikia popote ulipo.

3. Je, naweza kufanya nini ikiwa ninaomba msamaha kwa mtu lakini anakataa kunisamehe?

Huwezi kuwajibikia matendo ya watu wengine, unawajibikia tu kile unachofanya.

4. Je, Petro alikuwa ametoka wapi?

Petro alikuwa ametoka Galilaya

5. Je, Petro alifanya kazi gani kabla ya kuwa mwanafunzi?

Uvuvi

## Majibu kwa Darasa la Uendeshaji



### Je, maombi yanafanana vipi na picha hizi?

Simu ya Mkononi Ninaweza kuzungumza na Mungu katika maombi, kama kupiga simu. Mungu anaweza kunitumia ujumbe wa maandishi na naweza kusoma maandishi yake katika Biblia yangu. Hata kama sihisi hivyo, bado ninaweza kumwachia ujumbe. Yeye ataupokea.



Kuzama 1 Yohana 1:9 Ninaweza kukiri dhambi zangu na kutakaswa. Ninaweza kwenda kwake kwa maombi wakati ninayo kiu ya kiroho.



Kebo ya umeme Haina umuhimu isipokuwa imeunganishwa. Kuunganisha na Mungu kwa maombi kunaweza kunipa nguvu.

Jogoo Kama alivyofanya na Petro, Mungu anaweza kuzungumza nami kupitia chochote.






Je! anaweza kuwa anaomba kuhusu nini na anaweza kuwa anaomba msamaha kuhusu nini? Chora kwenye povu la wazo.









| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| O | G | O | P | A | N | Y | U | O | J |
| A | K | W | M | T | G | B | O | G | O |
| W | Y | I | B | A | U | S | E | Y | G |
| Y | Y | T | F | T | P | M | O | T | O |
| N | F | O | T | U | E | W | O | E | O |
| I | W | B | E | S | N | U | J | S | A |
| K | I | F | U | N | D | G | O | E | P |
| K | P | E | T | R | O | | U | K | W |
| S | A | M | A | I | K | A | M | A | S |


## Tayari, anza, Michezo!

Mbio za Kugongana (mchezo kwa Mtu binafsi)

Timu zote zinaweza kushiriki. Mtoto kutoka kila timu atachaguliwa na atakuwa ndiye atakayeweka wengine lebo. Ili kuondoa mtoto, mweke lebo mara 2. Wakati mwalimu anasema, "Nenda", mtoto aliyechaguliwa anatakiwa akimbize kila mtu na kujaribu kuwaweka lebo, wakati hili linafanyika, mtoto aliyetiwa lebo anapaswa kuweka mkono sehemu ambapo amewekwa lebo. Kwa mfano: ikiwa amewekwa lebo mgongoni au mguuni, anapaswa aweke mkono juu ya mgongo au kwenye mguu na aendelee kukimbia, akijaribu kutoroka. Mradi mkono mmoja haujawekwa lebo, anaendelea katika mchezo. Mtoto anandolewa wakati anawekwa lebo mara ya pili.Mtoto anaweka mkono huo mwingine sehemu ambapo amewekwa lebo na kubaki bila kusonga mpaka mchezo ukamilike. Mshindi ni yule ambaye hataondolewa. Timu ya itakayoshinda inapata pointi.

Mbio za Mpira (mchezo wa Timu)

1. Timu za VBS lazima zichague kiongozi.
2. Washiriki wa kila timu wanaunda mstari takriban hatua moja kutoka kwa kila mmoja. Kiongozi atakuwa hatua mbili mbele ya wengine.
3. Kila kiongozi anapewa mpira (karatasi iliyokunjwa, kwa mfano).
4. Weka alama angalau mita kadhaa kutoka mahali pa kuanzia (kiti, kwa mfano), ambayo wanaizunguka wakati wa mbio.
5. Mchezo unaanza wakati kiongozi atarusha mpira kwa mshiriki wa kwanza katika safu.Mtu huyo anakimbilia alama akiwa na mpira, anazunguka alama na kurudi. Anapofika kwenye safu iliyo na wenzake, anapaswa arushe mpira kwa kiongozi.Kisha anapaswa kukaa chini.
6. Kiongozi anarusha mpira kwa njia sawa kwa washiri wote wa timu.Wakati washiriki wote katika timu yake wanaketi, inapaswa pia yeye akimbie na azunguke alama.
7. Mchezo unakwisha wakati kiongozi wa timu anafika na kuketi kwenye mstari .
8. Timu ya kwanza kumaliza inashinda.
9. Ili kucheza tena, teua kiongozi tofauti katika kila timu



## Hitimisho

Leo imekuwa siku ya kwanza ya ajabu sana ya Shule yetu ya Biblia ya Likizo! Tumekuwa na wakati mwafaka wa kujifunza jinsi Petro alivyofanya kosa kubwa kwa kumkana Bwana wake wakati alikuwa chini ya shinikizo. Lakini alishinda dhambi yake kwa kuikubali na kukiri.Sote tunaweza kujifunza kutoka kwa Petro na kutambua makosa yetu na kukiri dhambi zetu mara kwa mara. Kwa njia hii, tunaweza kuweka "oili" ikiwa safi katika injini zetu na kukimbia mbio ya maisha ili tushinde!







# 2 Kumtii Mungu

Hadithi ya Biblia: Nuhu Anatii / Mwanzo 6:9-14, 7:1-24



## Fungu

“Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake.” 1 YOH. 2:3

## Mchezo wa Kuigiza

**Badiliko**

• Fundi wa gari ameketi mezani na mke wake anaandaa kifungua kinywa wakati binti yake anaingia.Msichana ni mwema kuliko kawaida na anasamilia kila mmoja kwa kikofi wazi na kisha wote watatu wanagandishwa.

• Mtangazaji anaingia na kuwaambia watoto kuwa fundi na mke wake hawajui, lakini wamembadilisha binti wao aliyekuwa muasi kuwa binti mzuri, binti Mkristo.Kisha anasema, "Tutaona tofauti."Fundi na familia yake wanaacha kuganda na wanaendelea na kuigiza mchezo huo.

• Kitu cha kwanza ambacho mama anatambua ni nguo za binti yake. Anauliza kama walimwomba shuleni avae mavazi ya kuigiza. Pia anamwuliza aliwacha wapi kipini chake cha puani na nguo ambazo kawaida huvaa. Binti anamletea babake gazeti pamoja na kahawa.

• Anazungumzia jinsi alivyomaliza kazi yake ya nyumbani na jinsi alisomea mtihani. Fundi anauliza kama anahitaji pesa kwa ajili ya kitu fulani, lakini binti anajibu hapana.

• Wazazi wanazungumzia kuhusu jinsi wanavyopenda binti yao jinsi alivyo sasa, na wanafurahia sana kuishi naye.Wakati wa kuondoka, binti anachukua zawadi ili kumpa mwalimu wake.

• Na binti anaondoka, fundi na mkewe wameketi, wameshangaa, wakijiuliza nini kimetendeka. Fundi anawaza,"Msichana huyu ni nani, na alimfanyia binti yetu nini?"

• Mtangazaji anarudi, akisema kwamba waliona tofauti; na ilikuwa wazi kwamba walipenda mabadiliko. Mtangazaji anamaliza kwa kutoa maoni ya kubadilisha watoto waasi kwa ajili yake Kristo.

### Kupata Umakini

Msemaji: “Je, utamtii Mungu?”
Watoto: “Nitatii…” (piga makofi, piga makofi na “Nitatii” kisha gusisha mikono kwenye miguu)
“Nitatii…” (piga makofi, piga makofi na “Nitatii” kisha gusisha mikono kwenye miguu)
“Nitamtii Mungu!” (piga makofi, piga makofi na “Nitatii” kisha gusisha mikono kwenye miguu mara mbili na “nitatii” kisha elekeza juu na “Mungu”)

## Ujumbe

Karibu tena kwenye mbio, watoto... na katika VBS "Washa Injini zenu!" Leo tutajifunza kuhusu sehemu nyingine muhimu ya mbio za pikipiki: matairi. Katika mbio, matairi ya pikipiki ni muhimu sana! Ni wazi kwamba pikipiki haiwezi kwenda bila matairi, lakini pia yanafaa yawe na mgusano mwafaka!!! Mgusano mzuri kutoka kwa matairi husaidia pikipiki kujishikilia kwenye lami vizuri, ili isiteleze barabarani.Katika mbio, washindani huweka matairi







MAPYA kwenye pikipiki kabla ya kuanza. Kwa hatua hii, wana hakika kuwa na mgusano mzuri katika mbio inayofuata.


Kumtii Mungu kwa kila namna ni kama kuwa na matairi mapya kwenye pikipiki yako, na kuwa na mgusano mzuri katika barabara yako. Ikiwa unataka kufika mahali fulani katika maisha, na unataka kufanya kitu KIKUBWA kwa ajili ya Mungu, unahitaji mgusano mzuri. Je, hii ina maana kwamba unahitaji nini? UTIIFU Dunia inatuambia kwamba tunapaswa kusimama kidete, na tuamini nafsi zetu kama tunataka kufanya kitu kikubwa, lakini Mungu anatufundisha kwamba tunahitaji kuwa watiifu na kufuata amri zake. Badala ya kuamini katika nafsi zetu, tunahitaji kuamini katika Mungu wa ajabu tunayemtumikia. Anatupenda sana, na anataka kutufikisha mahali fulani muhimu katika maisha!Utiifu utahakikisha kwamba tuna matairi ya kupiga hatua katika maisha yetu.Leo tutajifunza somo kuhusu utiifu wa mtu mzuri sana aliyeishi zamani, Nuhu. Aliendelea kumtii Mungu hata kama miaka mingi ilipita, na hakuwa na sababu ya kumtii Mungu. Lakini hii lina maana gani kwako na mimi?

Tunajua maana ya kutii wazazi wetu - inamaanisha kufanya kile wanachosema. Lakini inamaanisha nini kumtii Mungu? Tutajuaje anataka nini ilhali hatumwoni wala hatumskii? Njia kuu tunayoweza kumtii Mungu ni kwa kutii amri zake katika Biblia. Hapo tutapata masomo mengi kuhusu jinsi ya kuishi na jinsi ya kuwatendea wengine, jinsi Yesu alivyofanya.Pia, Mungu ameweka mamlaka juu yetu kwa manufaa yetu. Kwa hivyo, huwa pia tunamtii Mungu wakati tunatii wazazi wetu, walimu wetu, au wachungaji wetu. Wakati mwingine, Mungu pia hutupatia amri ya kibinafsi. Wakati mwingine, katika roho yetu tunajua kwamba tunapaswa kumsaidia mtu, kumpa kitu, au kuwa na huruma kwa mtu. Wakati wowote tunapopata jukumu maalum katika Maandiko kama vile amri kutoka kwa Mungu, na wazazi au mchungaji wetu anakubaliana na hili, tutajua kwamba tunaweza kufuata amri hiyo, na hii italeta furaha kwa Mungu. Tutafanya kitu maalum kwa maisha yetu tunapomtii Mungu; tutaweka matairi mapya kwenye pikipiki zetu za kukimbia... na tutapata mgusano fulani katika maisha. Hebu tufuate Mungu na mfano wa Nuhu kwa kuitii Biblia, mamlaka zetu, na sauti ya Roho Mtakatifu ndani yetu. Wavulana na wasichana, hebu kimbieni mbio hii ili kushinda na kwa kutumia baadhi ya mgusano!

## Mchezo wa Kujuana

Umeme

Gawanya wanafunzi wako katika timu mbili au nne. Idadi ya timu inategemea ukubwa wa kikundi chako .Unda mistari inayoangaliana. Weka kitu kati ya mistari. Wanafunzi wanashika mkono wa mtu aliye karibu nao. Kiongozi atashika mkono wa mvulana na mshichana wa kwanza katika kila timu (unahitaji kiongozi mmoja kwa kila timu mbili).





Kiongozi atafinya mkono ya mtoto wa kwanza wa kila timu. Mkono wako ukifinywa, unapaswa kufinya mkono wa mtu mwingine anayefuata katika mstari na kadhalika kwa haraka iwezekanavyo. Timu ya kwanza ya kumaliza na kuchukua kitu kilichowekwa katikati inashinda.Ikiwa unataka kuongeza msisimko zaidi, fungeni macho yenu.

## Somo la Biblia

Nuhu Anatii

1. Baada Mungu kuumba dunia, watu walianza kuongezeka na kulikuwa na watu zaidi na zaidi.Watu walikuwa wengi, lakini watu wakamsahau Mungu aliyewaumba. Pia wakasahau kumtii Mungu na wakafanya tu kulingana na maslahi yao wenyewe; kusema uongo, kuumizana na hata kuua wengine. Hawakujali kile Mungu alichotaka na hili lilifanya Munguawe na hofu.




Kwa neno, watu: Kwa kidole chako cha kati na cha gumba zikishikana, unda miduara inayobadilishana.




2. Katikati ya uasi huo kulikuwa na mtu ambaye alimpenda na kumtii Mungu.Jina lake lilikuwa Nuhu. Siku moja Mungu aliamua kumaliza watu wote wasiotii kwa kutumia mafuriko.Kwa hivyo Mungu alimwambia Nuhu kwamba atatuma dhoruba kubwa. Wakati huo hakuwahi kunyesha mvua duniani na hivyo Nuhu hakufahamu mvua ni nini.Ni lazima ilikuwa vigumu kwa Nuhu kutii kitu ambacho hakufahamu wala kuelewa. Mungu alimwambia Nuhu, "Itakuja mvua mpaka dunia yote itafunikwa na maji, lakini nataka uunde safina, (meli kubwa sana) kwa ajili yako, familia yako, na wanyama niliowaumba ili kuingia na kuwa salama humo ndani."

Kwa neno, kutii: Shikilia ngumi zako karibu na paji la uso wako; zishushe huku viganja vikiangalia juu.

3. Mungu alimwambia jinsi ya kujenga safina, aina ya mbao ambazo angetumia na ukubwa wake.Ukubwa ulikuwa mkubwa kuliko uwanja wa soka. Nuhu akaanza kufanya kazi na mbao kwa kukata na kuweka misumari. Nuhu na familia yake walifanya kazi nyingi, miaka mingi ili kutengeneza meli kubwa sana. Je! unaweza kuwaza ilivyokuwa kumtii Mungu kwa miaka na kufanya kitu ambacho huelewi, na kujiuliza jinsi Mungu atakavyotimiza yale aliyoahidi?



Kwa neno, Mungu: Kidole cha kulia cha shahada kinakuwa juu; Na kushusha na kufungua mkono kwenye kifua.



4. Siku moja Mungu akamwambia Nuhu, "Ingia ndani ya safina pamoja na familia yako na uruhusu wanyama wote waingie pamoja nawe." Kwa mara nyingine Nuhu akatii, aliweka chakula kwa wanyama wote na kwa familia yake. Mungu aliwatuma wanyama wote na wakapanda ndani ya safina, ikiwa ni pamoja na wanyama wakubwa na wadogo. Mwishoni, Nuhu na familia yake waliingia. Ghafla akaanza kusikia matone ya mvua, mvua ikaanza kuanguka na ikaendelea kuongezeka, Mungu akafunga mlango.

Kwa neno, familia: Huku vidole gumba na vidole vya shahada vikigusana, unda mduara unaoelekea nje mpaka mikono igusane.

5. Mvua ilikuwa tayari kali sana, madimbwi yakwa makubwa, mara baada ya muda duniani ikafunikwa na maji na mafuriko na safina ikaanza kuelea. (chora uso wa maji na mawingu). Ilinyesha kwa siku 40 na usiku 40. Mvua ilikuwa kubwa kiasi kwamba hata milima mirefu zaidi ilifunikwa na maji.Mpaka siku moja ikakesha na kila kitu kilikuwa kimya, mvua ilikuwa imekwisha. (chora jua) Ilichukua karibu mwaka ili ardhi ikauke kabisa.Siku moja, Mungu alimwambia Nuhu kwamba familia yake na



wanyama wangeweza kuondoka kwenye safina.Ilikuwa siku ya kusisimua kwa kuwa na uwezo wa kuwa nchi kavu tena! Nuhu na familia yake wangeweza sasa kukimbia, kunyorosha miguu yao kwenye jua.
Kwa neno, mvua: Mikono kwa mfano ya kikombe ikiwa imeinuliwa juu; Unda mizunguko ya miduara kwa pande.



6. Kitu cha kwanza ambacho Nuhu alifanya ni kumshukuru Mungu kwa kumweka salama. Mungu alifurahishwa na shukrani hizo kutoka kwa Nuhu na pia aliahidi kwamba "hatawahi tena kuharibu dunia kwa maji."Hivyo ili kutukumbusha ahadi hio, Mungu akaweka upinde maridadi wa mvua mbinguni. Nadhani Mungu alifurahishwa sana na Nuhu kwa kumtii, ingawa hakuelewa kila kitu ambacho Mungu alimwomba. Kila wakati unapoona upinde wa mvua, kumbuka kwamba Mungu aliuweka kama ishara kwamba hatawahi kuharibu dunia kwa maji tena.Inaweza kuwa vigumu kwako kutii Mungu, lakini kumbuka kwamba Mungu atatusaidia ikiwa tunamwomba. Anatupenda na anataka kutuonyesha upendo wake kila wakati tunapomtii.
Kwa neno, asante: Weka ncha za vidole vya mikono yako miwili kwenye mdomo wako na unyooshe mbele na chini.

# Vituo vya mzunguko

**Gawanya katika vikundi 3 ili waende katika vituo**

## Usanifu wa Gereji




Helmeti ya dereva wa pikipiki
Sambaza kwa kila mwanafunzi:
Karatasi 1 iliyochapishwa helmeti iliyo na maandiko ya kibiblia
Kipande 1 cha povu ya bluu au karatasi
Vipande 2 vya povu ya manjano au karatasi
Kipande 1 cha mapovu ya kijani au karatasi
Pini 1 ya usalama
Maagizo:
• Kwa karatasi ya povu/rangi na helmeti iliyochapishwa, unda kiolezo.
• Unapokuwa umezipanga inavyofaa, zigundishe katika sehemu mwafaka.
• Weka pini ya usalama ili waweze kuzipachika kwenye nguo zao.

## Sehemu ya Vitafunio



Gari ya Tufaha

*Viungo:*

- Tufaha
- Zabibu kavu au zabibu za zambarau
- Vijiti vya kuchokoa meno

*Maagizo:*

1. Kata tufaha katika hilali (nusu-mduara)
2. Weka vipande vya tufaha katika umbo la hilali vikiwa vimeangalia chini
3. Weka vijiti vya kuchokoa meno kwenye tufaha, kimoja upande wa mbele na kingine nyuma.
4. Weka zabibu au zabibu kavu kwenye ncha za vijiti vya kuchokoa meno, na kuiga matairi.

*Tayari!! Sasa tumeunda gari tamu sana.*


## Darasa la Uendeshaji

Karibu kwenye "darasa la uendeshaji gari" ambapo tutatumia vitabu vyetu vya wanafunzi. Je, tunaweza kuanza darasa kwa kurudia kwa pamoja somo la siku na fungu la siku? Tuanze!!!

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | B | M | V | U | A | J | I | O | M | K |
| O | M | N | U | H | U | N | Z | M | B | M |
| K | S | K | A | J | I | E | A | V | A | U |
| I | A | E | L | M | K | F | U | W | O | N |
| R | F | Z | A | E | A | K | A | K | B | G |
| U | I | O | L | G | I | Y | O | D | Z | U |
| F | N | E | N | R | F | A | N | J | H | J |
| A | A | E | M | A | J | I | R | A | N | I |
| M | J | A | B | I | M | J | M | A | W | A |

### Rejelea Biblia na uangalie ikiwa taarifa ni kweli (K) au uongo (U).

1. Nuhu anaishi miaka 350 baada ya mafuriko ( jumla ya miaka 950). Mwanzo 9:28-29 — (K) U
2. Mungu alimpa Nuhu upinde wa mvua kuahidi kuwa hakutawahi kunyesha mvua tena. Mwanzo 9:12-16 — K (U)
3. Kulikuwa na 14 ya kila wanyama walio safi katika safina. Mwanzo 7:2 — (K) U
4. Hatujui wazazi wa Nuhu walikuwa kina nani. Mwanzo 5 — K (U)
5. Methusela (mtu mzee zaidi katika Biblia, miaka 969) alikuwa babu wa Nuhu. Mwanzo 5:25-28 — (K) U
6. Ilichukua miaka zaidi ya 100 kujenga safina. Mwanzo 7:6 — (K) U
7. Kulikuwa na jozi 1 ya kila aina ya ndege ndani ya safina. Mwanzo 7:3 — K (U)



Je! unaweza kupata wawili kwa kila mnyama?Weka alama ya mduara kwenye wanyama ambao bado wanasubiri wenzao.Bila kuangalia, ni wanyama wangapi unaweza kutaja kutoka kwenye picha hii ndani ya dakika 1?



## Maswali na majibu

1. Ni nini kinafanyika ikiwa wakati wazazi wangu hawana haki?
Maisha hayana haki, kwa mfano, ikiwa kuna tetemeko la ardhi, linaathiri watu walio katika eneo hilo wawe ni wazuri au wabaya. Ukosefu wa haki mara nyingi hutokea, hata katika manyumbani mwetu. Je, kunaweza kuwa na njia ya kutii wazazi wetu, hata kama wanatuomba tufanye kitu kibaya? Mungu anaona kila kitu, hata kama wazazi wetu hawaoni. Mfano mmoja: uongo.
2. Je! Mungu amewahi kukuomba ufanye kitu? Ulijuaje kwamba amri ilitoka kwa Mungu?
Wakati mwingine tunahisi kwamba tunapaswa kwenda kumsaidia mtu, au tunasikia kuwa mtu fulani anatusumbua, au anatukumbusha kila wakati kuhusu jambo ambalo tunafaa kufanya. Mungu anatukumbusha kwa sababu hata wakati tunapojaribu kusahau, hatuwezi. Wakati mwingine tunaota ndoto kuhusu kitu tunachopaswa kufanya.
3. Je! unajiona kama mtiifu kwa Mungu?
Jaribu kuwa na majadiliano ya wazi na watoto wako, ambapo hakuna yeyote anahukumu mwingine. Shiriki makosa yako mwenyewe ili uwasaidie kujihisi sawa kuongea pia. Jadili matendo ambayo yanaashiria utiifu na matendo ambayo yanaashiria uasi.
4. Je, ni watu wangapi ambao waliingia ndani ya safina?
Wanane.
5. Watoto wa Nuhu walikuwa nani?
Shemu, Hamu na Yafeti

## Tayari, anza, Michezo!

**Kushikwa na Lori la kuvuta (Mtu binafsi)**
Kabla ya kucheza:
• Chagua mtoto (lori la kuvuta) ambaye atashika pikipiki (watoto wengine).
• Weka mipaka ya nafasi ya mchezo.
Kucheza:
Pikipiki zinakaa ndani ya mipaka iliyobainishwa na lori ya kuvuta inakimbia, ikijaribu kuzishika. Anaposhika pikipiki kwa mkono wake, pikipiki itashikisha mkono wake kwa mchezaji. Huku pikipiki ikiwa imeshikishwa mkono wake, lori ya kuvuta itajaribu kukamata kila moja ya pikipiki iliyosalia ili kuunda mnyororo.
Ikiwa mtu ataondoka mipaka iliyobainishwa, anapaswa kujaribu kujiunga na lori ya kuvuta.








Kumbuka: Wakati kikundi ni kikubwa, inaweza kuwa muhimu kuunda minyororo 2 na kutakuwa na lori 2 za kuvuta ili kuwezesha kushikwa kwa pikipiki.

**Mbio ya Kupokezana (Timu)**

Kwa mbio hii ya kupokezana, funga watoto wawili pamoja kwa mguu mmoja kila mmoja.
Unda timu, jaribu kuweka idadi ya washirika ikiwa inalingana katika kila timu.
Unda njia katika eneo la kucheza, moja kwa kila timu.
Kwa ishara, jozi ya kwanza inakimbia na kuzunguka njia, kisha ya pili, na kadhalika, mpaka timu nzima imekimbia.
Timu ya kwanza inakuwa washindi.



# Hitimisho

Leo imekuwa siku ya kusisimua ya Shule yetu ya Biblia ya Likizo! Tumekuwa na wakati mzuri na tumejifunza kwamba Nuhu hakusikia tu sauti ya Mungu, bali pia alikuwa na mgusano mzuri kwenye matairi yake katika maisha yake kwa kutii Neno la Mungu. Sote tunaweza kujifunza kutoka kwa Nuhu na kumtii Mungu mara kwa mara katika maisha yetu. Kwa njia hii, tunaweza kuweka "matairi" mazuri kwenye "pikipiki" zetu ili tuharakishe na tukimbie mbio ya maisha ili tushinde!

# 3 Upendo wa Kweli

Hadithi ya Biblia: Ruthu anapenda / Ruthu 1: 1-4:17

## Fungu

“Maana, hii ndiyo habari mliyoisikia tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi.” 1 YOH. 3:11

## Mchezo wa Kuigiza

Upendo

- Fundi anaingia akizungumzia kuhusu mteja ambaye alikuja na pikipiki yake kwenye gereji kwa sababu ilikuwa na joto jingi.Moshi inatoka kwenye pikipiki. Fundi anaanza kazi, akisema, "Haingepata joto jingi, kama ungeweza kutumia bidhaa ya kudhibiti halijoto katika injini. Sasa sijui ikiwa naweza kuitengeneza. "
- Wakati huo, mbwa wake mdogo anaingia na kuanza kuzungumza naye.Fundi anaangalia upande na upande, anashwangazwa na kila kinachozungumza naye. Anachukua muda akiangalia hadi anatambua kuwa ni mbwa ambaye anazungumza naye.
- Mbwa anathibitisha kwamba kwa kweli ni yeye anayezungumza naye kwa kumweleza hadithi kadhaa ambazo ni mbwa wake pekee anayeweza kuwa anajua. "Je! unakumbuka wakati ambapo mke wako alikuandalia chakula maalum cha jioni na ukamwambia kuwa ndicho chakula cha jioni chenye ladha zaidi maishani mwako, na baada ya kukula kijiko kimoja, ukanipa hicho kingine?"
- Hatimaye, fundi anaamini mbwa wake mdogo, na wanaanza kuzungumza kuhusu jinsi mbwa wote wanavyoweza kuzungumza, lakini wanaficha. Wanapokuwa wakizungumza, bado fundi anatengeneza pikipiki.
- Fundi anaelewa kuwa sababu ambayo mbwa wake alizungumza ni kwa sababu leo alitaka kumshukuru kwa upendo wake na huduma yake yote, kisha anachukua muda wa kumwosha upendo na kukumbatia. Kisha mbwa anaondoka.
- Mchezo wa kuiga unakwisha fundi akisema kwamba injini imeharibika kwa sababu imeongeza joto zaidi na kwamba mmiliki atahitaji kununua injini nyingine.
- Wakati fundi anaondoka, anasema, "Angekuwa tu akiilinda injini yake kwa bidhaa ya kudhibiti halijoto, bado ingekuwa na maisha marefu ya kutumika."

### Kupata Umakini

Msemaji: “Izungushe!”
Watoto: Piga makofi mara tatu
Piga makofi mara tatu
“Vroom, vroom!” (mikono kama inazungusha mafuta ya pikipiki)
“Twende!” (ngumi ya kulia juu na kisha ngumi ya

## Ujumbe

Habari watoto... mko tayari kuzungusha injini zenu???
Nani atashinda mbio hii hata hivyo? Je, unaweza kuendesha pikipiki yako kwa kasi ya juu zaidi? Ikiwa huwezi, basi unastahili uondoke barabarani, kwa sababu pikipiki ni bora zaidi zikiwa mbioni.

Wakati wa kukimbia, injini ya pikipiki huongeza joto sana... na bidhaa ya kudhibiti halijoto ni muhimu sana ili kulinda injini kutokana na joto la juu. Kwa hivyo leo, tutajifunza kuhusu bidhaa ya kudhibiti halijoto! Hiki ni kioevu ambacho unaweka kwenye rejeta badala ya maji. Hiki huzunguka ndani ya injini, na huiweka baridi, hata wakati inaendeshwa kwa kasi sana. Bila hii, injini inaongeza joto na huanza kutoa moshi, wakati mwingine hata huwaka moto!Hakuna namna ya kushinda mashindano ya pikipiki ambayo inaongeza joto. Je! hii inahusuje maisha yetu ya kiroho? Upendo katika maisha ya Mkristo ni kama bidhaa ya kudhibiti halijoto katika pikipiki. Kutakuwa na mvutano kati ya watu wakati wote. Mungu alitufanya sisi wote kuwa tofauti na kuwa na tofauti nyingi za maoni na tabia. Wakati hatuna upendo katika maisha yetu, tunaweza kuingia katika migogoro na kutoelewana.Je, umewahi kuona watu wawili ambao kwa kawaida huishi vizuri wakigombana? Ndiyo, kila mtu! Hata katika makanisa makubwa, matatizo hutokea na Mungu anatarajia tuonyeshe upendo kwa kila mmoja. Bila Upendo, moshi utaanza kutokea katika maisha yetu, au kutoka kanisa letu, na moto utaanza. Na muhimu zaidi, ikiwa mimi na wewe hatutaonyesha upendo kwa wengine, tutaongeza joto hata zaidi na hatutaweza kushinda mbio.

Kwa nini bidhaa ya kudhibiti halijoto ni muhimu sana? Naam, Biblia inaonyesha kwa uwazi kuwa upendo ndio sifa kuu ambayo tunapaswa kutumia katika maisha yetu ya Kikristo.Je, ina maana gani kuonyesha upendo kwa wengine? 1 Yohana 3:16 inatusaidia kuelewa upendo: *"Hivi ndivyo tunavyojua upendo ni: Yesu Kristo alitoa maisha yake kwa ajili yetu."* Biblia inasema kwamba sisi pia tunapaswa kutoa maisha yetu kwa wengine, lakini kwa jinsi gani? Hii inamaanisha kuchukua kipande kile kidogo cha keki, kujitolea ili rafiki yako awe wa kwanza kucheza kwenye mchezo, kusaidia wazazi wako hata wakati hawajakuomba, kumngojea rafiki baada ya shule, kuwa mzuri kwa mtu shuleni hata wakati hawana uzuri, na mengi zaidi.Je, ni kwa njia ngapi tunaweza kuonyesha upendo wa kweli kwa wengine? Orodha haikamiliki! Baada ya kugundua njia ya kuonyesha upendo, tunapaswa kutambua umuhimu wake.Sio kitu tu tunachohitaji kufanya pamoja na orodha ya mambo ya kidini tunayofanya: kuhudhuria kanisa, kutoa sadaka na kutii wazazi wetu. Yesu anaweka wazi katika Agano Jipya kwamba "dini" yako haifanyi kazi ikiwa huna upendo kwa wengine - kutoa maisha yako na kuweka wengine kwanza.

Leo tutakwenda kuangalia dereva wa ajabu wa mbio... Ruthu. Anatupa mfano mzuri wa jinsi ya kutoa maisha yako kwa ajili ya mtu mwingine.

Tutaendelea kujali maisha yetu ya Kikristo, ili tuweze kumtumikia Mungu kwa muda mrefu. Hebu tuonyeshe upendo kwa wengine na tushinde mbio hii!

## Mchezo wa Kujuana

**Nambari na Vitendo**

Waombe wanafunzi waunde timu, za watu kumi hadi kumi na wawili, ikiwa inawezekana. Kumbuka kwamba watoto wadogo na wanafunzi wakubwa wanaweza kushiriki katika timu moja.Timu zitasimama, kila mwanafunzi mbele ya mwenzake. Ikiwa hutaki kuhamisha watoto, unaweza kufanya shughuli kama wameketi.

Eleza kwamba kila nambari itakuwa na kitendo.


1. Kumpatia mwenzetu kikofi cha juu.
2. Kuchuchumaa.
3. Kuruka juu kama tumeinua mikono.
4. Kugeuka.
5. Kosonga huru (hapa unaweza kucheza baadhi ya nyimbo).





Kiongozi anasema namba na wanafunzi watafanya kitendo kinacholingana. Wote wanaochanganyikiwa wakati wa kufanya vitendo lazima wakae chini, lakini kumbuka kwamba lengo la michezo ni kujuana ni kuleta ushirikiano. Furaha ndio jambo muhimu zaidi.

## Somo la Biblia


**Ruthu Anapenda**



1. Ruthu alikuwa msichana mrembo wa Kimoabu (kutoka eneo ambalo linajulikana kama Moabu) aliolewa katika familia kutoka Israeli ambayo iliishi Moabu. Ruthu na mumewe waliishi katika nyumba ya familia ya mumewe.Baada ya muda, baba ya mumewe alifariki na kisha mumewe na mume wa dadake mkwe pia walikufa. Na sasa Ruthu, dadake mkwe, na mama mkwe, Naomi, walisalia peke yao kwa sababu wote watatu walishakuwa wajane (waume wao walikuwa wamefariki).
Kwa neno, mume: Funga vidole vya mkono wa kulia wakati unavyoondoka kutoka kwa kichwa chako.Shika mikono yako.




2. Katika siku hizo kwa mwanamke ambaye hakuwa na mume, maisha yalikuwa magumu sana. Ilikuwa vigumu kwake kufanya kazi ili kujitegemea. Wanawake watatu labda waliwaza, je, ni nani atakayetusaidia sasa tangu waume wetu wamefariki? Naomi aliwaambia binti zake wakwe,"Nendeni mkae pamoja na familia zenu, labda mtaolewa tena huko, lakini mimi nitarudi katika nchi yangu ya Israeli." Hawakutaka kumwacha Naomi, lakini mwishowe dadake mkwe wa Ruthu aliamua kuondoka na kurudi nyumbani kwa familia yake.
Kwa neno, ondoka: Kwa mikono yako ikiwa imefunguliwa upande wa chini na uifunge unapoiinua juu.



3. Ruthu hakutaka kumwacha peke yake na akamwambia, "Nitakwenda pamoja nawe!Nitakuwa binti yako, watu wako watakuwa watu wangu na Mungu wako atakuwa Mungu wangu." Naomi akagundua kwamba Ruthu alikuwa ameamua na hangeweza kubadili mawazo yake, hivyo Ruthu akaenda pamoja na Naomi hadi Bethlehemu (mji ambao Naomi aliishi hapo awali). Wakati huu hawakuwa na waume, walikuwa na furaha kwamba angalau walikuwa pamoja na walikuwa wakiishi pamoja.
Kwa neno, pamoja na: Funga mikono yako, na uweke ngumi zako pamoja.



4. Walipofika Bethlehemu, wakulima walianza kuvuna shayiri, huku wakikata mimea ya shayiri. Ruthu akaanza kukusanya shayiri iliyoanguka nyuma ya wavunaji, wanaume ambao walifanya ukataji, kwa sababu hakuwa na mume wa kumsaidia pamoja na Naomi. Bibilia inasema kwamba nafaka na mabua yanayoanguka chini, na mimea inayokua katika pembe za shamba, zinapaswa kuachwa ili kuwalisha maskini, kwa hiyo akachukua mabua yaliyoanguka. Hivyo, Ruthu alifanya kazi ya kukusanya mimea baada ya uvunaji ili waweze kupata chakula.
Kwa neno, mimea: Unda mduara na vidole vyako vya mkono wa kushoto, unapotumia mkono wako wa kulia kuingia ndani ya mkono wa kushoto.




5. Ruthu alifanya kazi kwa bidii nyuma ya wavunaji kwa muda mrefu, hakujali joto jingi. Naomi alikuwa mzuri sana kwake; alikuwa amemsaidia, na hivyo Ruthu alitaka kuhakikisha kwamba alikuwa mzuri kwa Naomi pia.Ndiyo sababu alikuwa akifanya kazi kwa bidii ili kuleta chakula cha kutosha kwa Naomi.








Kwa neno, mzuri: Mkono wa kushoto ukiwa katikati, songesha mkono wako wa kulia kutoka juu hadi chini.



6. Shamba ambalo Ruthu alikuwa akikusanya nafaka lilimilikiwa na jamaa ya Naomi. Jina lake lilikuwa Boazi. Boazi alipomwona Ruthu akifanya kazi, akamwuliza mfanyakazi wake, "Yeye ni nani?" Mfanyakazi akamwambia, "Ni mwanamke kutoka Moabu aliyekuja pamoja na Naomi. Aliniuliza kama ningemruhusu aweze kufanya kazi, kukusanya tu mabua ambayo yalianguka chini.Amekuwa akifanya kazi kwa bidii tangu asubuhi." Boazi alikuwa amesikia jinsi Ruthu alivyomtendea Naomi tangu walipowateza waume zao.Boazi akamwambia kwamba angeweza kuchukua mabua yoyote aliyotaka, na hakuna mtu angemsumbua, na kwamba angeweza kufanya kazi katika mashamba yake.
Kwa neno, kazi: Kwa mikono yako ikiwa imefungwa, gusa mkono wako wa kushoto kwa mkono wako wa kulia.

7. Ruthu alikusanya mabua wakati wote wa mavuno. Naomi alipotambua kuwa alikuwa akifanya kazi katika shamba la Boazi aliyekuwa jamaa yake, alipanga mpango wa hekima. Mpango huo ulikuwa yeye na Ruthu waweze kuokoa sehemu ya ardhi ya familia yao. Naomi alimwambia Ruthu kuhusu mpango huo.Kwa hivyo, Boazi alirudisha shamba ambalo lilikuwa la Naomi, na sasa Naomi na Ruthu wakapata shamba. Boazi alimwoa Ruthu na wakati walipopata mtoto wa kiume walifanya sherehe katika nyumba ya Naomi. Kupitia mpango wa hekima, Naomi na Ruthu wakapata manyumbani na familia zao tena.
Kwa neno, hekima: Kwaruza paji la uso wako kwa kidole cha mkono wako wa kulia.



8. Licha ya kifo cha mume wa Ruthu, aligundua kwamba Mungu alitaka amtii na aonyeshe upendo wake kwa watu wengine.Ilikuwa uamuzi mkubwa kwa Ruthu kutoacha mamake mkwe peke yake, lakini kurudi pamoja naye Israeli. Huenda usijue jinsi ilivyo kwenda kufanya kazi ya kukusanya mabaki ya mavuno, lakini nina hakika unajua jinsi ya kuwa mzuri kwa watu wengine, hata wakati ni vigumu. Mungu atakubariki wakati unapenda wengine kwa sababu sio tu jambo jema la kufanya, lakini pia ni jambo la hekima zaidi. Pia tunajifunza kwamba hata katika hali ngumu, Mungu huweka karibu nasi watu ambao tunapaswa kuwaonyesha upendo wa Mungu.

## Vituo vya Mzunguko

**Gawanya katika vikundi 3 ili waende katika vituo**

### Usanifu wa Gereji

Miwani ya Mashindano ya Gari
Sambaza kwa kila mwanafunzi:
Karatasi 1 yenye muundo wa miwani
Mshipi 1 wa karatasi nyekundu ya selofeni senitmita 18 x 3.5
Utepe au kamba ya sentmita 50




- Kata eneo jeupe kutoka kwa miwani na miduara kwenye kingo.
- Panga rangi unayopenda kwenye miwani yako.
- Kwenye upande wa nyuma, funga kipande chako cha selofeni, ili ifunike sehemu ya katikati ya miwani

• Funda utepe katika kila shimo ili zitoshee kwenye kichwa cha mwanafunzi.

## Sehemu ya Vitafunio

**Sandiwichi yenye umbo la moyo**



Viungo:

• Mkate mweupe
• Kifaa cha kukata kidakuzi katika umbo la moyo au karatasi ya wastani ya umbo la moyo
• Chupa yenye jemu ya stroberi
• Kisu (ikiwa huna kifaa cha kukata kidakuzi)
• Kijiko cha plastiki

Maagizo:

1. Tengeneza mikate ya kutosha yenye umbo la moyo.
2. Paka jemu katika nusu ya mioyo ya mikate.
3. Weka moyo mwingine wa mkate juu ya ulio na jemu.

*Tayari!! Sasa tuna sandiwichi tamu ya kufurahia!*

## Darasa la Uendeshaji

Karibu kwenye "darasa la uendeshaji gari" ambapo tutatumia vitabu vyetu vya wanafunzi. Je, tunaweza kuanza darasa kwa kurudia kwa pamoja somo la siku na fungu la siku? Tuanze!!!



## Maswali na majibu

1. Kwa nini Mungu hawezi kuondoa watu wote wabaya duniani?
Mungu anapenda kila mtu na anaendelea kutarajia kuwa kila mtu atatubu dhambi zake na kumrudia. Kutaka Mungu aondoe watu wote waovu inaweza kuwa hatari sana kwa sababu sisi wote tuna uovu fulani uliofichwa mioyoni mwetu, kwa hiyo tunaweza kuangamizwa pia!
2. Je! tunapaswa kuwa rafiki na kila mtu?
Lazima tuwapende wengine, kuwa wazuri na wenye urafiki na kila mtu. Hata hivyo, ikiwa mtu anakuwa mkatili, si lazima tuwe rafiki yake. Tunapaswa kuonyesha upendo kwa maadui zetu, lakini hatuhitaji kuwa marafiki wao wakati wote.
3. Je, ni lazima niweke mahitaji ya wengine mbele ya mahitaji yangu?
Ndio, tunapaswa kuwapa wengine kipaumbele kutuliko.Pia, ikiwa tunataka kuishi kama Yesu, lazima tuweke mbele maslahi ya watu wengine.

4. Mji wa Naomi ulikuwa mgani?
Bethlehemu ya Yuda, katika Israeli
5. Jina la binti mpwa mwingine wa Naomi lilikuwa gani?

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | K | U | S | A | N | Y | O | F | U | A | T | A | B |
| H | U | M | P | O | A | Z | I | D | P | F | N | Y | E |
| A | M | E | M | U | M | R | I | A | N | K | U | N | T |
| Y | F | H | A | T | I | T | B | E | A | E | Y | A | H |
| B | A | E | V | Y | I | M | K | U | O | O | P | S | L |
| O | I | L | A | S | A | M | A | Y | N | A | S | U | K |
| A | O | H | U | H | U | K | U | V | I | Z | F | K | E |
| Z | S | T | S | U | H | T | U | R | U | P | E | N | M |
| I | A | E | I | K | F | I | M | O | A | N | D | K | U |
| S | L | B | Z | I | B | T | H | L | A | M | O | U | E |

1. Nini kilichotokea kwa mume na wana wa Naomi? Walifariki.
2. Naomi aliwapa Ruthu na Orpa nini? Walichagua nini?
Kusalia Moabu. Orpa alirudi Moabu. Ruthu alikaa na Naomi.
3. Ruthu alionyeshaje upendo?
Alikusanya shayiri kwa ajili ya kutoa na kumtunza Naomi.
4. Naomi alionyeshaje upendo?
Alikaribisha Ruthu nyumbani mwake na alitaka awe pamoja naye.
5. Boazi alionyeshaje upendo? Alizungumza na mkombozi wa jamaa kwa ajili ya Ruthu na kisha akamuoa.


2

1

3

Andika namba katika masanduku ili uweke picha kwa utaratibu.



1

3

2

## Tayari, anza, Michezo!

**Kimbia!! (Mtu binafsi)**



Huu mchezo ni tofauti na mchezo wa "Lebo" wa kawaida.Katika mchezo huu ni muhimu kutia alama eneo la mchezo, na katika kila alama ya kona ni sehemu itakayotumika kama eneo salama (msingi au makao).

Mchezo unajumuisha yafuatayo:


Watoto wote wanaohusika wanapaswa kuwekwa ndani ya eneo la mchezo. Mtoto mmoja anachaguliwa kukimbiza wengine.Mwalimu akisema kwa sauti, "Kimbia," mtoto aliyechaguliwa anapaswa kukimbiza kila mtu, akijaribu kuweka lebo (kuwagusa), hili linapotokea mtoto aliyewekwa lebo anapaswa kuondoka kwenye mchezo. Wote wanapaswa kukimbia, wakitafuta nafasi katika eneo salama (msingi au makao) kwa sababu mahali hapo watakuwa salama na hawawezi kuondolewa kutoka kwenye mchezo. Mara kila mtu akiwa katika eneo salama, mwalimu anapaswa kusema tena, "Kimbia!". Kila mtu anapaswa kuondoka eneo salama na kuhamia kwenye makazi tofauti.Ikiwa wanakaa mahali sawa, wanapaswa kuondoka kwenye mchezo. Ikiwa wanatoka kwenye mstari au kikomo kilichowekwa, wanapaswa pia kuondoka katika mchezo. Mtoto asiyeondolewa anakuwa mshindi.

Timu ya itakayoshinda inapata pointi.

**Soka ya Kifagio (Timu)**

Kwa mchezo huu unahitaji timu 2 zinazoshiriki, vifagio 2 na mpira 1.

Weka malengo 2 nje na uchague moja kwa kila timu.
Timu 2 zinaundwa mbele ya kila mmoja na kila mshiriki anapewa nambari.
Hakikisha kuna idadi sawa ya washiriki katika kila timu.
Mpira pamoja na vifagio vinawekwa katikati ya uwanja.
Wakati kiongozi anasema nambari kwa sauti, mtoto aliye na nambari hiyo kwenye kila timu anapaswa kukimbia, achukue ufagio na ajaribu kuweka mpira kwenye lengo pinzani.
Gusa mpira na ufagio tu.
Baada ya kufunga bao, acha ufagio na mpira katikati.
Kiongozi anaendelea kuita nambari mpaka kila mtu acheze.
Timu inayofunga bao nyingi inashinda.
Kumbuka: Ikiwa hutaki kutumia ufagio, cheza jinsi unavyocheza mpira wa kandanda kwa kawaida.



## HITIMISHO

Leo imekuwa siku ya kusisimua ya Shule yetu ya Biblia ya Likizo! Leo tumekuwa na furaha nyingi na tumejifunza jinsi Ruthu alivyoonyesha upendo wa kweli kwa watu walio karibu naye, akijitolea kwa ajili ya wengine badala ya kuwa na wasiwasi kujihusu. Tumejifunza kwamba hii ni kama kuweka bidhaa ya kudhibiti halijoto katika gari letu, ambayo itauzuia kupandwa na hasira, ubinafsi, migogoro na kutoelewana. Tunapaswa kuweka "bidhaa ya kudhibiti halijoto" katika maisha yetu, ili tuweze kushinda mbio!

# 4 Kufahamu Nguvu



Hadithi ya Biblia: Danieli Anakutana na Nguvu / Danieli 6:1-28

## Fungu

“Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.” 1 YOH. 4:4

## Mchezo wa Kuigiza

**Fundi wa gari na Shujaa wa Kibiblia mwenye Nguvu**

• Fundi wagari anatembea ili kuchukua sanduku ambalo limewasili kwenye Ofisi ya Posta. Ni sanduku kubwa lililo na sehemu nyingi, ikiwa ni pamoja na injini na pampu ya mafuta. Pampu ni kwa ajili ya mteja ambaye alileta pikipiki yake, akisema kwamba pampu yake ya mafuta ilikuwa imeharibika, na kwamba alitaka mpya.

• Anaanza kucheka kwa wasiwasi. Kisha anaona shujaa mwenye nguvu zisizo za kawaida akijiongelesha. Anajaribu kuwaza anaweza kuwa nani na pia anaona sanduku lililo na sehemu za pikipiki.

### Kupata Umakini

Msemaji: “Kanyaga breki!”
Watoto: Kanyaga mara mbili kwa mguu wa kulia
“Err-err-errrt!” (sauti ya breki, mwendo utakuwa kikofi cha mkono kunyooshwa nje, kisha mkono huo mwingine, kisha mkono wa kwanza)
“Tayari kusikiliza!” (elekeza kwa sikio moja, elekeza kwa hilo lingine, kidole gumba kimeangalia juu)

• Mtu mwenye nguvu zisizo za kawaida, ambaye anaweza kusoma akili, anasema, "Mimi ni shujaa wa Kibiblia mwenye Nguvu, na niko likizoni." Wanazungumza kwa muda na fundi wa gari anaomba saini yake. Kwa kuwa shujaa mwenye nguvu ana macho ya eksrei, anaweza kuona ndani ya sanduku.

• Fundi wa gari anamwambia shujaa mwenye nguvu kwaheri na kisha anajaribu kuinua sanduku, lakini ni nzito sana. Anajaribu kwa nguvu zake zote, na miguu yake, na kila kitu kinachokuja mawazoni.Anajua kwamba shujaa mwenye nguvu anaweza kumsaidia ikiwa atamwomba.Fundi wa gari hataki kuomba usaidizi wa shujaa mwenye nguvu kwa sababu yuko likizoni. Anajaribu kuhamisha sanduku tena, analisongesha kidogo na kidole chake kinafinywa na anaanza kupiga kelele kwa maumivu. Hatimaye, anaamua hawezi kuliinua na anamwambia shujaa mwenye ngugu kwaheri.

• Kabla ya kuondoka, shujaa mwenye nguvu anamwuliza ni nini kilichokuwa kinashangaza kuhusu pampu ya mafuta.Fundi wa gari anamwambia kuwa amegundua kuwa pikupiki ilikuwa imeishiwa tu na mafuta na kwamba hahitaji pampu mpya. Wanacheka pamoja kuhusu mteja ambaye kwa mwezi wote amekaa bila kutumia pikipiki.

• Fundi wa gari anaondoka kwa sababu hawezi kuinua sanduku. Baadaye shujaa mwenye nguvu anatokea, na anainua sanduku kwa urahisi akisema, "Kitu ambacho ni cha kushangaza ni kwamba angeweza kuomba usaidizi."







## Ujumbe

Karibu tena kwenye VBS "Washa Injini zenu!"
Tunakaribia kumaliza, kwa hivyo tunahitaji kujua nani aliye na nguvu na ni nani ambaye hana. Leo tutazungumzia kuhusu nguvu! Nguvu inayofanya pikipiki hizi zikimbie kwa kasi ya haraka sana, ni mafuta (petroli)! Bila hiyo, pikipiki zitaonekana nzuri, lakini zitakuwa zimesimama, hazitaweza kusonga. Kama sote tunavyojua, petroli huhifadhiwa kwenye tenki kwenye pikipiki, na pikipiki hutumia mafuta yale inaposonga. Kwa wakati fulani, pikipiki itaishiwa na mafuta, na itasimama, kama haitawekwa mafuta mengine. Nguvu ya Mungu katika maisha ya Kikristo ni kama mafuta kwenye tenki zetu.



Mungu ndiye hufanya tusonge mbele na kutupa nguvu. Ni ajabu kugundua kwamba hatuongozwi na nguvu zetu wenyewe. Kila kitu kinachofanya maisha iwe ya kuvutia hutuunganisha na Mungu. Itakuwa ya kusikitisha ikiwa tutasimama katikati ya mbio katika sehemu fulani ya maisha kwa sababu tu tuliishiwa na mafuta!
Mojawapo ya kanuni za kusisimua zaidi katika Maandiko ni ukweli kwamba hatufai kuishi maisha ya Kikristo kwa nguvu zetu wenyewe - na kwa kweli hatuwezi! Wagalatia 2:20 inasema,"...si mimi tena ninayeishi bali ni Kristo anayeishi ndani yangu, " na Paulo anazungumzia waziwazi kuhusu jambo hili katika Warumi 7, " Nani ataniokoa kutoka kwenye mwili huu wa mauti?Asante kwa Mungu kwa ajili ya Yesu Kristo Bwana wetu."Tumepewa kazi isiyowezekana ya kuishi kwa ukamilifu kwa ajili ya Mungu, hata ingawa dhambi inatujaribu kila mahali. Uzuri wa hili ni kwamba Mungu anatujua, hata katika udhaifu wetu; na Yeye hutusaidia kwa niaba yetu!Anatupa nguvu tunayohitaji ili kukamilisha kazi aliyoweka mbele yetu. Anapigana na adui kwa ajili yetu; anaenda kabla yetu na kutuongoza katika vita.Tunaweza kupumzika kwa nguvu zake! Pia inasisimua kujua kwamba Mungu wetu ni mkubwa zaidi kuliko miungu mingine yoyote, na ni mkubwa zaidi kuliko adui yetu Shetani na pepo zake zote. Kwa muda mfupi, Mungu amempa Shetani ruhusa ya kuzunguka dunia hii, lakini Mungu bado ako kila mahali, bado ana nguvu kuliko mtu yeyote, ingawa ameruhusu shetani awe na nguvu kidogo juu ya dunia. Fungu letu la kumbukumbu la leo linatangaza, "... aliye ndani yenu ni mkubwa kuliko aliye katika dunia." Leo tutakutana na Danieli, mtu wa Biblia ambaye aliweza kuona nguvu za Mungu zikifanya kazi!
Hatupaswi kamwe kuishiwa na nguvu au mafuta ya Mungu, lakini tukumbuke kuendelea kukaa kama tumeunganishwa Naye! Baadhi ya njia za kusalia kama tumeunganishwa Naye ni kupitia maombi, kusoma Biblia, kuhudhuria kanisa, na kusikiliza wale wanaoshiriki ushuhuda wao nasi. Njia bora ni moja kwa moja kutoka Kwake hadi kwako. Je! umejaza tena tenki yako ya mafuta hivi karibuni?

## Mchezo wa Kujuana

**Nambari ya siri**

Wachezaji wanachagua nambari, 1, 2, 3, 4 au 5.

Hawana mwongozo wowote wa kujua nambari gani wanapaswa kuchagua; kila mmoja anawaza kuihusu kwa sekunde chache na anaamua ni gani atakayochagua.

Hawapaswi kuisema kwa sauti kwa mtu yeyote anayecheza.

Wachezaji wanaondoka mahali pao, wanachanyanyana na kuanza kusalimiana kwa mikono bila kusema chochote. Watoto wanaunda vikundi wanapopata watoto wengine wenye nambari inayolingana na yao.Kumbuka mchezo huu unafanyika bila kuzungumza. Ikiwa mchezaji amechagua namba 1, basi atasalimiana mkono mara moja pekee. Ikiwa umechagua nambari 3 basi unapaswa kusalimiana mara tatu na usubiri mchezaji huyo mwingine pia









akusalimie mara tatu kwa mkono ili ujue kama walichagua namba sawa na yako. Ikiwa wana nambari sawa, wanajiunga nawe na kuendelea kutafuta wengine wenye nambari sawa.Wachezaji wanapaswa kubaki kimya. Kundi la kwanza la wachezaji kuunda timu kamili litakuwa mshindi.

## Somo la Biblia

**Daniel Apatana na Nguvu**



1. Danieli alikuwa kijana ambaye alipelekwa kwenye kasri ili kumtumikia mfalme, na alifanya kazi yake kwa uhodari hadi akafanywa kuwa afisa. Alikuwa mwaminifu na alipenda kumtii Mungu. Kila siku alimwomba Mungu huku madirisha ya chumba chake yakiwa wazi; aliomba mara tatu kwa siku, na hakuomba tu wakati wa chakula pekee.
Kwa neno, Mungu: Inua kidole chako cha gumba cha kulia, kisha ufungue mkono wako unaposongesha mbele ya kifua chako.



2. Mfalme Dario alifurahishwa na kazi njema ambayo Danieli alikuwa akifanya, na akaamua kumweka Danieli kuwa msimamizi wa kila kitu. Baadhi ya maafisa walijawa na hasira sana kwamba Mfalme Dario amemchagua Danieli kuwa msimamizi (chora nyuso zenye hasira za wanaume). Maafisa wenye hasira walianza kupeleleza Danieli ili kutafuta jambo ambalo wangetumia ili kufanya mfalme aache kumpendelea, lakini, hawakupata chochote kibaya! Walipoona Danieli akiomba mara tatu kwa siku kwa Mungu, wakapata wazo kuu (Chora balbu za mwangaza juu ya vichwa vyao).
Kwa neno, hasira: Kwa vidole viwili vya mkono wako wa kulia, visongeshe mbali na uso wako.



3. Maafisa kwa ujanja wakafanya mfalme Dario aunde sheria mpya.Sheria ilisema kwamba kwa siku 30, hakuna mtu aliyepaswa kuomba kwa mungu yeyote ila kwa Mfalme Dario. Mtu atayekaasi atatupwa katika shimo la simba, na kama kila mtu anavyojua, hakuna mtu aliyeweza kuishi katika shimo la simba wenye njaa. Maafisa wenye hasira walikuwa na uhakika kwamba simba wangeweza kumuangamiza Danieli. Walijiuliza pia kama Danieli angeweza kuacha kumwomba Mungu.
Kwa neno, simba: Tingisha mkono wako wa kulia ulikunjwa juu ya kichwa chako; songesha mkono wako nyuma.



4. Mara moja, Danieli alisikia kuhusu sheria mpya. Daniel angeweza kujificha katika chumba chake, au afunge dirisha ili asionekane, au angeweza kuacha kuomba kwa siku hizo 30 kwa Mungu. Lakini maombi yalikuwa ya umuhimu sana kwa Danieli, ambaye aliendelea kumwomba Mungu kwa njia ile ile kama alivyofanya hapo mbeleni (mara tatu kwa siku kama madirisha yamefunguliwa). Mara tu wale maafisa wenye hasira walipomwona, walikwenda kumwambia mfalme habari kwamba Danieli amevunja sheria.
Kwa neno, sheria: Songesha vidole vilivyopindana vya mkono wako wa kulia chini kwa urefu wa mkono wako wa kushoto.







5. Mfalme Dario akajawa na hasira sana, sio kwa sababu Danieli alikuwa ameasi sheria, lakini kwa sababu aligundua kuwa maafisa walikuwa wamemdanganya ili kumlaumu Danieli. Shetani alikuwa amewatumia na ilionekana kama angeshinda. Katika Babiloni, mara moja mfalme alitoa amri, lazima ingefuatwa na haingeweza kubadilishwa. Mfalme Dario alijua kwamba sheria hii ya kipumbavu lazima ingetimizwa bila mtu yeyote kuomba.Kwa hofu nyingi, aliandamana na Danieli kwenye shimo la simba.



Kwa neno, omba: Gusa vikofi sehemu ya mbele; songesha mikono yako kwenye mwili wako na uinamishe kichwa chako.

6. Mfalme Dario akamkumbatia Danieli, akamwambia, "Natumaini kwamba Mungu wako anaweza kukuokoa kutoka kwa vinywa vya simba hawa wenye njaa," na baada ya hayo Danieli akatupwa katika shimo la simba. Wakaweka jiwe kubwa ili kufunika lango la shimo, na mfalme akaweka muhuri juu ya jiwe ili mtu yeyote asiliondoe. Usiku huo, mfalme alikuwa na wasiwasi mwingi kuhusu Danieli; hakuweza kulala.Alitumia usiku wote akitembea ndani ya chumba chake, akijiuliza kama Mungu alikuwa na uwezo wa kutosha wa kumwokoa Danieli. Mapema sana asubuhi, mfalme akakimbilia kwenye shimo, akaondoa muhuri, akafungua mlango na akaita Danieli, "Danieli, Mungu alikuokoa?"Kisha akasikia sauti kutoka kwenye pango," Ndio, Mungu aliniokoa kutoka kwa simba, aliamuru malaika wake kufunga vinywa vya simba." Mfalme aliamuru askari wamwondoe Danieli kutoka kwenye shimo la simba. Mfalme Dario siku hiyo akatoa amri nyingine, ambayo alisema kuwa Mungu wa Danieli ndiye alikuwa Mungu wa kweli. Kisha aliwaadhibu maafisa wenye hasira.



Kwa neno, mfalme: kidole cha gumba cha kulia kati ya kidole cha shahada na kidole cha katikati; songesha kutoka kwa bega hadi kiuno.

## Vituo vya Mzunguko

**Gawanya katika vikundi 3 na uende kwenye vituo**

### Usanifu wa Gereji

Sambaza kwa kila mwanafunzi:
Tenki 1 ya mafuta iliyochapishwa
Nozeli 1
Mikono 2 ya karatasi
Riboni 1, sentimita 35
Kisafishaji 1 cheusi cha kusafisha bomba, kata katika sehemu 3 sawa




- Waombe wanafunzi wako wapake rangi vipande kwa rangi wanazopendelea.
- Gundisha visafishaji viwili vya kusafisha kwenye nyuma ya upande ili viwe mikono na katika sehemu ya mwisho ugundishe mikono miwili.
- Weka kisafishaji kingine cha kusafisha bomba katika sehemu ya chini na upande huo mwingine uweke nozeli.

• Kata riboni katika sehemu 4 na uziweke kwenye sehemu ya nyuma ili kuunda nywele. Pia kwa mkasi unaweza kufanya baadhi ya misokoto ili ufanye ivutie zaidi.

## Sehemu ya Vitafunio

Chupa ya maji yenye ladha



*Viungo:*

• Chupa 1 ya maji ya mililita 200
• Pakiti na ladha ya Kijamaika, ladha ya Tang, nk kwa ajili ya maji
• Mshipi 1 wa karatasi iliyochapishwa na kiolezo cha muundo mweusi na mweupe (sentimita 6 kwa 15)
• Gundi ya aina yoyote inayopatikana
• Kitafunio unachopendelea

Maagizo:

1. Fungua chupa ya maji
2. Fungua pakiti ya ladha
3. Weka baadhi ya unga katika chupa ya maji, funga na utikise chupa
4. Gundisha mshipi wa karatasi katikati mwa chupa
5. Ikiwa unapendelea: Patia mtoto kitafunio pamoja na kinywaji

Furahia kitafunio cha kupendeza!

## Darasa la Uendeshaji

Karibu kwenye "darasa la uendeshaji gari" ambapo tutatumia vitabu vyetu vya wanafunzi.Mbona tusianze darasa kwa kurudia pamoja somo la siku na fungu la siku?Tuanze!!!



### Waza kuwa wewe ni Danieli. Andika:

Majibu yanaweza kutofautiana na bado yawe sahihi. Hapa kuna mifano michache:

Mambo 5 unaweza kuona:
Kuta za shimo,
simba,
mfalme,
meno ya simba,
hakuna njia ya kutorokea.

Mambo 4 unaweza kugusa:
Shungi la simba,
Kuta za mawe,
Uso wangu kuifuta jasho,
Vidole vya miguu yangu.

Mambo 3 unaweza kusikia:
Simba anakoroma,
Upepo nje,
Upumuaji wangu wenye uoga

Vitu 2 unaweza kuhisi vikinukia:
Jasho langu,
Na simba hunuka!

Kitu 1 ambacho unawaza:
Mungu wangu ni mwenye nguvu sana!

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H | A | T | S | I | M | B | A | U | K |
| U | D | R | I | N | I | A | M | U | T |
| M | S | I | L | E | I | N | A | D | O |
| U | A | B | R | S | R | B | L | H | M |
| N | N | L | H | I | U | K | A | O | B |
| G | A | I | A | D | S | T | S | D | A |
| U | M | T | U | I | A | H | I | A | L |
| O | U | G | K | R | K | H | A | R | I |
| S | H | M | I | U | T | A | T | I | G |







## Maswali na majibu

1. Je, itakuwaje tukihisi kana kwamba kwamba Mungu yuko mbali nasi?
Inahitaji imani kumwamini Mungu wakati hatumwoni wala kumsikia.Hata hivyo, bila kujali jinsi tunavyohisi, Mungu yupo, anatupenda na anatujali.
2. Je, kwa nini Mungu huruhusu mambo mabaya yatendeke?
Kwa ajili ya ukuaji wetu wa kiroho na ili tuweze kuwasaidia wengine kuamini (hatuwezi kusaidia sana isipokuwa kama tumepitia matatizo pia). Wakati dhambi iliingia ulimwenguni, iliathiri kila mtu. Mungu hakuweka ukuta mkubwa kuwazunguza Wakristo. Sisi sote tunaishi katika ulimwengu mmoja, tunashiriki sayari sawa, na tunapaswa kuwepo na tayari kusaidia wengine.









3. Je ni mambo gani yanayokutia uoga?
Zungumza kuhusu mambo mbalimbali, kama vile buibui na kuhama hadi shule tofauti.Jaribu uwafanya wajisikie huru ili waweze kushiriki uoga wao. Usijaribu kupata majibu kwa kila uoga, sikiliza tu na uwaache washiriki.
4. Je, Mfalme Dario alifanya nini baada ya kumweka Danieli kwenye shimo la simba?
Alifunga kula na kunywa.
5. Je ni nani alitupwa ndani ya shimo la simba wakati Danieli alipotolewa?
Wanaume waliomshtaki Danieli.

## Tayari, anza, Michezo!

Bendera Nyeusi (Mtu binafsi)
(Daraja tofauti za London)
1. Watoto wanaunda mzunguko mkubwa iwezekanavyo.
2. Mbele na kama wameshikana mikono, watoto 2 wanaunda daraja au handaki huku mikono yao ikiwa imeinuliwa.
3. Kwa sauti ya muziki, watoto watatembea kwa mwelekeo wa saa, kupitia kwenye handaki.
4. Wakati anayeongoza mchezo anasema kwa sauti, "Bendera nyeusi!" muziki unasimama. Watoto wawili wanaounda handaki wanashusha mikono yao, na kumkamata mmoja ya watoto.



5. Watoto wawili watapokamatwa watatengeneza handaki nyingine mbali na ile iliyotangulia.
6. Handaki zinaundwa mpaka kuna mshindi.
Kumbuka: Unaweza kuongeza msisimko kwenye mchezo kwa kucheza muziki tofauti, kubadilisha mwelekeo unaozunguka, kuruka kwa mguu mmoja, kuruka kidogo, kurudi nyuma, nk.
Timu ya Eneo la Salama (Timu)
Timu zote zinashiriki. Toa puto kwa kila timu. Kila timu inapaswa kuwa na idadi sawa ya washiriki.
Kila timu imewekwa katika safu wima na kuacha nafasi kati ya kila timu.
Wakati msimamizi anasema kuanza, wanaanza kupitisha puto kutoka mbele na nyuma. Wa kwanza atapitisha juu ya kichwa chake, anayefuata chini ya miguu yake, na kubadilisha kwa namna hiyo hadi puto ifikie mwisho wa mstari.
Mtu wa mwisho akipokea puto, anatembea kinyumanyuma kama amefunga macho yake, akijaribu kufika mwanzoni mwa mstari.Timu inasaidia tu kwa kusema maelekezo.
Wakati mtu huyo anapofika mbele, anza mzunguko tena.
Timu ya kwanza kufanikiwa kupitisha safu nzima inashinda.



# Hitimisho

Leo imekuwa siku ya kusisimua ya Shule yetu ya Biblia ya Likizo! Tulifurahia kujifunza jinsi Mungu alivyomwokoa Danieli kutoka kwa simba!Kwa njia hiyo hiyo, bila "mafuta" katika injini zetu, bila nguvu za Mungu, hatuwezi kwenda popote! Lakini kwa nguvu za Yesu Kristo ndani yetu, tunaweza kufanya mambo ya ajabu kwa ajili ya Mungu, na kukimbia mbio kwa haraka jinsi tuwezavyo ili kushinda.

# 5 Wokovu Usioweza Kunyimwa

Hadithi ya Biblia: Yesu Anatuokoa / Mathayo 27:32 - 28:10



## Fungu

“Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.” 1 YOH. 5:13

## Mchezo wa Kuigiza

Dereva

• Max ni dereva wa kushindana, na yuko katikati ya mbio muhimu sana.Anatumia redio yake kuzungumza na fundi mkuu kuhusu maelezo ya mbio.Max anasema: "Ndiyo, naona... Ninakwenda polepole kwa angalau zamu moja," anaangalia kwenye kioo na kubadilisha kasi na kuipunguza.

• Wakati huo huo, fundi mwingine wa gari ambaye tunamfahamu tayari ako karibu na fundi wa Max, anaanza kuinua kichwa mara kadhaa ili watoto wamwone, lakini ako makini ili fundi wa Max asimwone.Max anaangalia hali ilivyo mbele yake na anamwuliza fundi mkuu nini cha kufanya.

• Fundi huyo anayejificha anachukua redio nyingine na kuharibu mazungumzo, kwa sauti kubwa anamwambia Max maoni yake wakati anaangalia. Max anaingiwa na wasiwasi na anajaribu kuwasiliana na fundi wake ili amwambie kuwa mtu mwingine anatumia redio.

• Fundi anaanza kutoa maagizo kwa maskini Max, ambaye anajaribu kusikiliza kiongozi wake na hawezi kumwelewa kwa sababu anasikiliza watu wawili kwa wakati mmoja.

• Fundi huyo mwingine anazungumza kana kwamba anafahamu maelezo ya mbio na jinsi ya kushughulikia pikipiki, lakini Max anaanza kuzungumza kuhusu uzoefu wake kama dereva na pia kuhusu fundi wake mkuu.Fundi huyo mwingine anasema kwamba hata yeye anajua, na kwamba ameona mashindano mengi kwenye televisheni na kwamba pia yeye ni fundi kama fundi wa Max.

• Katika hatua hii katika mchezo wa kuigiza, fundi huyo mwingine anajaribu kuwa mtaalamu sana lakini anaongeza sauti yake ili ifanane na ile ya fundi mkuu ili Max aweze kufuata tu sauti yake.

• Max anapiga kelele kwamba hawezi tena kuvumilia hili na kumwambia fundi huyo mwingine kwamba atasikiliza ushauri wa fundi wake pekee na sio mtu mwingine.Kwa hili, Max anamkaribia na kuondoa redio kutoka mkononi mwake. Haraka, fundi huyo mwingine anaomba saini ya Max.Max anampigia kelele na kurudi kwenye mbio haraka.

### Kupata Umakini

“Nani hukuokoa?”

Watoto: Piga makofi, makofi, makofi “Yesu!” (elekeza juu kulia, elekeza juu kushoto)

## Ujumbe

Katika mbio za pikipiki, ni muhimu sana timu kuwa na kiongozi. Pikipiki zina wamiliki, wafadhili, na pia kiongozi wa timu.Mtu huyu huchaguliwa kulingana na ustadi na sifa zake. Dereva mzuri wa pikipiki hawezi







kushinda bila kiongozi mzuri kwa sababu husaidia dereva afanye maamuzi sahihi na aweze kuona hali yote ya mchezo.Je! hili linahusuje maisha yetu ya Kikristo?
Leo tutajifunza kuhusu wokovu. Je, ina maana gani kukubali zawadi ya Yesu ya wokovu? Ina maana kwamba sisi tubadilishe maisha yetu kwa ajili yake.Ina maana kwamba tumwombe Awe kiongozi wa maisha yetu. Ni kama kumwomba Yesu awe kiongozi wa timu yetu. Tumwombe achukue jukumu katika maisha yetu, ili tuweze kudhibiti vizuri maisha yetu ya baadaye.
Mungu alituumba na kutuweka humu duniani, lakini kuna dhambi zinazotuzunguka kila mahali.Ingawa hatutaki, wengi wetu hutenda dhambi kila siku, dhambi ndogo hadi kubwa.Biblia inasema kwa wazi kwamba malipo ya dhambi zetu ni mauti (Warumi 6:23)! Kwa hiyo, nini kitatundekea?
Unapofanya mambo mabaya, hii haimaanishi kwamba utakufa wakati huo huo! Hii ina maana kwamba wakati tunapokufa, tutahukumiwa kwa kufanya uovu, na tutatumwa kuadhibiwa pamoja na shetani. Hii inaonekana kutisha, lakini ni mbaya sana kuliko tunavyoweza kuwaza! Hata hivyo, Mungu kwa huruma zake, alifanya mpango na akamtuma Mwanawe duniani ili afe msalabani na kulipa dhambi zetu.Kifo chake kilikuwa mahali petu! Kwa kweli, leo tutasikiliza kuhusu hadithi hii ya kushangaza!




Lakini tunaweza kufanya nini? Yote tunayofaa kufanya ni kukubali dhambi zetu na kuamini kwamba Yesu ndiye ambaye alisema kuwa ndiye, Mwana wa Mungu.Tunapokiri dhambi zetu na kuamini, tunapokea zawadi - wokovu!Hii inamaanisha kwamba "tumeokolewa" kutokana na adhabu ya milele katika jahanamu, na tutafurahia mbinguni pamoja na Yesu kwa milele daima! Hii ni habari njema!
Je! umewahi kutoa kitu na kisha kukichukua tena? Tunafanya hivyo kwa Mungu wakati wote. Tunasema, "Nitafanya chochote Unachotaka nifanye," lakini tunapoenda shuleni, tunafanya kile tunachotaka badala ya kile Anachotaka. Tunapomwomba Yesu awe kiongozi wa maisha yetu, tunapaswa kuacha maisha yetu mikononi mwake! Maisha yetu yatakuwa bora sana ikiwa tutafanya hivyo, tutaweza kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutoharibika, na pia tunaweza kushinda mbio!Hebu tumwachie Yesu awe kiongozi wa timu!

## Mchezo wa Kujuana

**Salamu na Mduara wa Maswali**

Unda miduara miwili, mmoja ndani ya mwingine, kwa idadi sawa ya wanafunzi (bila kujali umri au urefu, unaweza kuchanganya wanafunzi). Ikiwa unataka, mchezo huu pia unaweza kufanyika bila miduara.
Miduara miwili inakwenda katika mwelekeo kinyume wakati muziki unacheza. Wakati muziki umesimama, kila mtu atakuwa na mshirika mbele yake, atasema , "Hujambo", na jina lao na kujibu mojawapo ya maswali yafuatayo.




- Ni chakula gani unachopenda zaidi?
- Je! Unaweza kukariri fungu la Biblia kutoka Somo la 2?
- Ni mhusika yupi wa kibiblia unapenda katika VBS hii?
- Je, ni shughuli gani unapenda zaidi katika VBS?
- Je, umekutana na mtu mpya katika VBS hii? Sema jina lake.

Rudia mchakato huu, na kuanzisha muziki na kuusimamamisha tena ili jozi mpya ya wanafunzi iweza kuuliza maswali kwa kila mmoja.








## Somo la Biblia


**Yesu anatuokoa**



1. Marafiki wa Yesu walikuwa na hofu na huzuni.Usiku mmoja kabla, umati wa watu wenye hasira ulikuwa umemkamata Yesu na kwenda naye. Yesu alikuwa amehukumiwa kifo - ingawa Yesu hakuwa amefanya chochote kibaya.
*Kwa neno, Yesu: gusa vikofi vya mikono yako kwa vidole viwili vya kati vya mkono huo mwingine.*




2.Askari wa Kirumi walimfanya Yesu abebe msalaba mgongoni mwake, pia wakampiga kwa nguvu sana kiasi kwamba hangeweza kutembea. Walipofika mahali pa kusulibiwa kwake, askari walimpigia Yesu misumari kwenye msalaba. Hata vibaya zaidi kuliko maumivu ya kimwili, watu walimtukana, wakamtemea mate, na kumtendea vibaya. Yesu alitupenda sana kiasi kwamba alivumilia majeraha na adhabu zote mpaka akafariki msalabani na kututakasa dhambi zetu, hata wakati angeweza kuwazuia. Hivi karibuni giza ikaingia, ingawa ilikuwa mapema mchana. Baada ya hapo kulikuwa na tetemeko la ardhi, na dakika chache baadaye Yesu akafariki msalabani. Ilikuwa ya kutisha sana!
*Kwa neno, msalaba: songesha mkono wa kulia upande wa chini kama umepindwa ndani; kisha kutoka kushoto kwenda kulia.*



3.Yesu alizikwa kaburini baada ya kufariki. Siku tatu baadaye, wanawake kadhaa walikwenda kaburini asubuhi na mapema, lakini walipofika kaburini, waligundua kwamba mwamba mkubwa wa kuzuia kaburi ulikuwa umeviringishwa upande mmoja. Wanawake walishangaa sana!
*Kwa neno, mwanamke*: kidole cha gumba cha mkono wa kulia uliofunguliwa kinagusa kindevu na kisha kifua.



4.Mmoja wa wanawake, Maria, hakujua cha kufanya kuhusu kaburi tupu, kwa hiyo akakimbia kwenda kumwona Petro na Yohana, marafiki wawili wa Yesu. Alipowaambia, walikimbia kaburini. Walipoingia, hawakumwona Yesu. Mwili haukuwa tena ndani ya kaburi! Petro na Yohana hawakujua kilichokuwa kimetendeka.
*Kwa neno, kaburi: Mikono bapa inasonga kutoka mabegani na kushikana katikati.*




5. Maria, ambaye aliyekuwa amewafuata hadi kaburini, aliendelea kulia. Alipoingia kaburini tena, lilikuwa tupu, lakini kulikuwa na malaika wawili ambao walimwuliza, "Kwa nini unalia?" Maria akawajibu malaika: "Kwa sababu mwili wa Yesu haupo hapa," akawaambia, "Sijui wamempeleka Yesu wapi." Alipoondoka kwenye uwepo wa malaika, Maria alikuwa karibu kumwangukia mtu, lakini alidhani alikuwa mmoja wa wafanyakazi katika bustani.
*Kwa neno, malaika: vidole kwenye mabega; viondoe na uvisongeshe juu na chini.*









6. Kisha akasikia sauti ikimwita, "Maria!" Mara moja akaitambua sauti - alikuwa Yesu. Hapa Alikuwa, mbele yake, na alikuwa hai. Yesu akamwambia aende akawajulishe wengine, alikimbia kama amefurahi sana, akalia kwa sauti kubwa, "Yesu yuko hai, nimemwona," na kila mtu alishangaa. Kile Yesu alichokuwa amewaambia kabla kilikuwa cha ukweli.Mpango wa Mungu ulikuwa mzuri.Baadaye, Yesu aliwatokea marafiki zake, nao wakaanza kumwambia kila mtu habari njema, kwamba Yesu yu hai!
*Kwa neno, hai: vidole vya gumba na vidole vya mbele vikiwa vimenyooshwa, na kusongesha mikono juu ya mwili.*

Mwalimu: Hii ni nafasi nzuri ya kuwakaribisha watoto wamkubali Yesu Kristo. Waulize kama wanaamini Yesu Kristo kama mwokozi wao.Fanya hivyo mara kadhaa ili uwape fursa nzuri ya kujibu, kisha uwaalike warudie maneno haya baada yako: "Bwana Yesu Kristo, nakuamini wewe kama mwokozi wangu. Ninatambua kwamba nimetenda dhambi dhidi yako. Ninataka kutii na kukupenda na kupenda wengine. Ninataka nguvu yako ndani yangu. Ninataka kukupa maisha yangu. Wewe ni bwana wangu. Tafadhali kuja na uishi ndani ya moyo wangu. Asante, Bwana. Amina."







# Vituo vya Mzunguko

**Gawanya katika vikundi 3 na uende kwenye vituo**

## Sehemu ya Vitafunio



Pia ya Bisi

*Viungo:*

- Mfuko 1 mkubwa wa bisi
- Karatasi 1 ya rangi ya machungwa
- Gundi au utepe wa gundi

*Maagizo*

1. Kunja karatasi kimshazari na ukate sehemu za ziada, na kuunda mraba.
2. Unganisha kingo ya juu kushoto na kingo ya chini kulia, na kupishana kwa angalau sentimita 2 ili uweze kuunganisha mraba kwenye pia.
3. Kata sehemu za ziada ya kuunda umbo la pia.
4. Jaza pia na bisi.

*Tayari!! Sasa ni wakati wa kufurahia mbio.*

## Usanifu wa Gereji

**Medali**

Sambaza kwa kila mwanafunzi:

Karatasi 1 yenye medali iliyochapishwa.

Karatasi 1 ambayo sehemu yake ya chini ina medali iliyochapishwa.

Mapambo kidogo ya kumetameta kwa kila mtoto.




Medali:


- Kata mzunguko wa miduara miwili na mwingine wenye alama ya tairi, kuwa makini usikate vifungo, kisha upake rangi.
- Kunja vichupo vya mstatili kwa digrii 90.
- Kwa gundi kidogo, funga vichupo kwenye upande mmoja wa mstatili kwenye upande wa nyuma ya mduara, fanya vivyo hivyo na mduara huyo mwingine, ili uweze kuunda medali ya 3D.
- Pamba na na mapambo ya kumetameta.

Utako:

- Chukua karatasi yako yenye utako uliochapishwa, kata mstatili kutoka katikati, kunja maeneo yenye nukta na upake rangi.
- Gundua kuwa katika pembe kuna pembetatu mbili.Ziunganishe kwa ndani na uzigundishe pamoja.
- Hatimaye, weka medali yako katika nafasi uliyokata.

## Darasa la Uendeshaji

Karibu kwenye "darasa la uendeshaji gari" ambapo tutatumia vitabu vyetu vya wanafunzi. Mbona tusianze darasa kwa kurudia pamoja somo la siku na fungu la siku? Tuanze!!!





| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Y | S | A | L | I | K | U | F | A | V | M |
| E | D | H | M | W | H | Y | E | S | M | S |
| S | A | U | L | I | Z | A | W | A | B | A |
| U | P | A | B | T | N | Z | O | N | I | L |
| I | N | A | P | A | T | I | K | A | N | A |
| T | H | W | O | K | O | V | O | W | G | B |
| D | H | A | M | B | I | K | V | M | U | A |
| G | A | U | B | U | G | N | U | M | N | Z |
| U | I | L | A | Z | E | L | E | L | I | M |

Je! umesikiliza kwa umakini hadithi ya siku ya leo? Una dakika 1 ya kuandika maneno yote ambayo unaweza kuwaza kutoka kwa somo.
Mwalimu: mshindi ni yule mwenye maneno zaidi. Vinginevyo, wafanye watie alama maneno yoyote ambayo wanafunzi wengine wamewaza, na atakayebaki na maneno mengi yasiyo na alama anakuwa mshindi.
YESU, KUSULUBIWA, MSALABA, DHAMBI, LIA, PUMUA, MISUMARI, SHUTUMU...
YESU, KUSULUBIWA, MSALABA, DHAMBI, LIA, PUMUA, MISUMARI, SHUTUMU...







## Maswali na majibu

1. Je, uhai wa milele unamaanisha nini? Je! inawezekanaje kwamba tunaweza kuishi milele?
Kwa uhai wa milele, hakuna wakati; ni uzima usio na mwisho baada ya kifo.Biblia anasema kuwa sisi ni wa milele, kwamba tutaishi milele mbinguni au katika jehanamu.Hii pia ina maana kwamba hatutaweza kurudi duniani kama mtu au nafsi nyingine, kama wengine wanavyoamini, lakini tunapofariki tunaondoka duniani milele na milele.
2. Je, kwa nini sio kila mtu huamini Yesu?
Mungu aliwapa wanadamu uhuru wa kuchagua kama wataamini au la, kwa sababu alitaka tuwe na uhuru wa kuchagua, na tusiwe kama roboti zisizo na chaguo. Watu wengine hawajisikia mambo ya kutosha kuhusu Yesu ili









kujua cha kuamini. Wengine wamesikia mambo ya kutosha lakini wameamua kutoamini na kutofuata Yesu. Watu wengi huchagua kutomwamini Yesu kwa sababu itawalazimu wabadilishe maisha wanayoishi.
3. Je, Mungu huzungumza na sisi vipi? Je, kitu cha mwisho alichokuambia kilikuwa nini?
Mungu huongea nasi kupitia neno lake, Biblia.Mafungu yataonekana "kuruka" kutoka ukurasa na kuonekana kutumika katika hali mahususi.Mungu anaweza pia kutumia watu kama vile waelekezaji, wachungaji na walimu kuzungumza na wewe. Mungu anaweza pia kuzungumza nawe moja kwa moja kama vile unapohisi kwamba unapaswa kusimama na kumsaidia mtu au kuepuka hali fulani, mtu au mtaa.
4. Je, ni nini kilichotokea duniani kabla ya Yesu kufariki?
Ilijawa na giza mapema na kulikuwa na tetemeko la ardhi.
5. Je, ni mitume wagani waliokuwa wa kwanza kuingia kwenye kaburi la Yesu na kugundua kuwa hakuwepo?
Petro na Yohana

## Tayari, anza, Michezo!

**Zilizochomwa (Timu)**
Weka alama kwenye mraba wa mita 15x15. Gawanya watoto katika timu 4 za idadi sawa ya wachezaji katika kila timu. Kila timu inasimama upande wao wa mraba. Toa nambari kwa kila mtoto. Kwa mfano, mchezaji mmoja katika kila timu amepewa nambari 1, mchezaji mwingine katika kila timu anapewa nambari 2, nk.
Weka mpira katikati ya mraba. Hakikisha ni mpira ni laini sana kama watoto watapiga mpira.
Mwalimu anasema kwa sauti nambari fulani kwa nasibu, na mtoto kutoka kila timu ambaye alipewa nambari hiyo anakimbilia mpira kwenye katikati ya mraba. Mtoto ambaye anafikia mpira akiwa wa kwanza anauchukua na anashinda pointi kwa timu yake. Kisha wanajaribu kutupa mpira ili kugonga watoto kwenye timu hizo zingine kwenye makali ya kingo za mraba. Ikiwa wanafanikiwa, wanapata pointi nyingine kwa timu yao.
Baada ya kutupa mpira kwa mara ya kwanza, watoto wanne katikati ya mraba wanaweza kuendelea kukimbiza mpira na kuutupa kwenye timu pinzani. Ruhusu sekunde 5-7 kwa shughuli hiyo.
Muda unapokwisha, watoto wanaondoka na kuacha mpira katikati ya mraba na kurudi ili kujiunga na timu zao.
Mwalimu anasema nambari nyingine ili kucheza tena.
Weka kumbukumbu ya alama ili ujue mshindi ni nani.

Kweli/Uongo (Mtu binafsi)
Weka alama kwenye eneo katka sakafu au chini. Upande utajulikana kama Ukweli na huo mwingine utakuwa Uongo.
Andaa mistari ya ukweli na ya uongo mapema kutokana na masomo ya VBS, na pia hali mbalimbali za hadithi za kibiblia.
Katika mchezo huu, taja mambo kuhusu masomo.
Ikiwa wanafunzi wanawaza kuwa maneno hayo ni ya ukweli wanakwenda upande wa ukweli, au kama wanadhani ni uongo, wanakwenda upande wa uwongo.
Watoto ambao wanajibu vibaya wanaondoka kwenye mchezo.
Mshindi ni mtoto atakayekuwa wa mwisho.



# HITIMISHO

Tumekuwa na shule ya likizo ya Biblia ambayo imekuwa ya kusisimua sana! Katika wiki yote tumefurahia kujifunza jinsi ya kuweka mafuta katika injini wakati tunapokiri dhambi zetu, jinsi ya kuweka matairi mazuri kwa kutii Neno la Mungu, jinsi ya kuweka bidhaa ya kudhibiti halijoto kwenye gari ili tuwe na upendo juu ya maisha ya wengine, na jinsi tunavyohitaji nguvu ya Yesu kama mafuta ili kwenda popote. Leo ilikuwa sehemu bora zaidi: tulijifunza kwamba Yesu Kristo ndiye bwana wetu! Tunamkubali leo kuja mioyoni yetu na kutoa vitu hivyo vyote katika maisha yetu yote, kutuongoza na kutupa zawadi yake ya wokovu, ili tuweze kuwa mbinguni pamoja naye daima dawama! Tuna mbio ya kukimbia; Hebu tukimbie kwa kasi ya juu tukiwa pamoja na Yesu!





